# MASHUJAA WA IMANI

SHULE YA JUMAPILI




## KITABU CHA MWALIMU

Kwa umri wowo

# MASHUJAA WA IMANI

**Mtaala wa Shule ya jumapili kutoka "Watoto ni Muhimu"**

**Kitabu cha Mwalimu**

**Kwa umri wowo**

**Sehemu ya 2: somo 1-13 (14-26)**

**Tovuti: www.ChildrenAreImportant.com/heroes/**


## SHUKRAN KWA TIMU YOTE YA "WATOTO NI MUHIMU"

Editor: Kristina Krauss
Creative Team: Abril Palacios Camacho, Areli Zuriel Salinas Sanchez, Dwight Krauss, Jennifer Sánchez Nieto, Julio Sánchez Nieto, Mike Kangas, Monserrat Duran Díaz, Suki Kangas, Verónica Toj, and Vickie Kangas.
Thanks to Rubén Dario for the wonderful music in this program.
Translation Team: alineviera, Annupama Wankhede, Anton Klymyk, Araz Mammadzadeh, Aroma Publications and Media, Arturo Jr Boron, Blessy Jacob, Carmela Dawn Flores, Chrisbresnahan, David Raju, Ephraim Njuguna Mirobi, Finny Jacob, Geenav, HamidReza Azimi (hamid.azimi1364 at gm#ail com), Heyaudrey, I-clever.com, iqbalman, Jacob Kuruvilla, kamilturk, Karunguru Mwangi, kiran, Maitrayi Mondal, Marco Chu, Marcos Rocha, Mathew Das, Mitesh Mandaliya, mrramlama, Mrs.Geethashree NavaneethaKrishnan, Nassim Bougtaia, nicbenk, Paul Mwangi, Paul Septan, Rana922, Rubina Rai, Safdar Khan, shahroshan15, Talento-Unido, ueritom, Verdia Juliansyah Cancerika, Yeoh Jung Chin, Zeina Mirella Barzaga Arencibia

# UTANGULIZI

**¡KARIBU!** kwenye sehemu ya pili ya Shule ya Jumapili ya "Mashujaa wa Imani"!

Tukiendelea kusoma kuhusu "Mashujaa" mbalimbali kutoka Agano la Kale, ni vyema kuangazia ni wapi tunapoiweka imani yetu, na hapo ndipo tutaangazia Sehemu ya 2. Tunapokalia kiti, tunaamini kwamba kiti hicho kitatudumisha, na kwamba hakitavunjika na kutafanya tuanguke chini. Imani yetu ipo kwenye kiti hicho, katika nguvu zake, na kujua hivyo basi tunaendelea na kuketi. Ni Sawa na Mungu. Imani yetu ipo wazi na inaeleweka tukijua Mungu ni nani. Tunahitajika kujua Mungu ni nani, ili tuweze kumtegemea. Kama tunavyokitegemea kiti kutudumisha, tunafaa kujua Mungu ni nani, na kwamba anaweza kutushikilia maishani. Fungu la maneno la sehemu hii linasema kwamba kwanza tunafaa kuamini kwamba Mungu yupo. Kuna Mungu! Hatupo peke yetu katika ulimwengu huu, Mungu aliumba ulimwengu na akatuumba. Pili, tunafaa kuamini kwamba Mungu anawapa zawadi wanaomtafuta.Tunafaa kuamini Biblia inachosema kuhusu Mungu. Tutaingia moja kwa moja katika hadithi nyinginezo katika Agano la Kale, lakini sasa tutaangazia Mungu mwenyewe. Je, tunaweza kusoma kutoka kwa sifa za Mungu, yeye ni nani, na anavyofanya katika hali tofauti? Tunapoendelea kusoma kuhusu tabia za Mungu, na kuamini kila kitu, itaongeza imani yetu. Ni njia nzuri ya kumshukuru Mungu, kwa sababu andiko kuu pia linasema…

"Na pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu kwa maana kila mtu anayemjia ni lazima aamini kuwa yupo na kwamba yeye huwapa tuzo wale wanaomtafuta ka bidii. " Waebrania 11:6

Tumejumuisha maswali ya kutosha mara tatu, kucheza "Mchezo wa Mashujaa" katika sehemu hii. Tunaupendekeza mchezo huu katika somo la 4, 8 na 13. Kwa mfano, chukua saa moja baada ya somo la kawaida au ucheze katika siku nyingine wiki hii. Kama walimu, tumia mchezo huu kama njia nyingine ya kuwafunza watoto.

Ili kukupa msaada, tumerudia taswira na maelezo ya Sehemu ya 1, jinsi ya kutumia nyenzo hii na sehemu mbalimbali za nyenzo hii. Tunatumaini hili litakusaidia tena katika kutumia programu hii darasani, kwa ajili ya kuleta mabadiliko katika maisha ya watoto.

Katika sehemu hii, tunakuhimiza kwenda mbele ya Mungu mwenye uwezo wote aliyeumba ulimwengu, aliyeishi na kuhusika katika Agano la Kale, na ambaye hivi leo yupo hai na yupo miongoni mwetu. Mungu abariki maisha yako kwa kuelekeza watoto walio karibu nawe ili waone maisha ya Mashujaa wa imani!

Kwa Upendo,
Timu ya Watoto ni Muhimu








# JINSI YA KUTUMIA NYENZO HII

## HADITHI YA UHITAJI/ SULUHISHO

"Mwalimu bora sio yule anawapa wanafunzi wake maarifa, lakini yule anayefanya waelewe umuhimu na wawe na hamu ya kutafuta maarifa." -MJ Berrill

**RATIBA**

**kufungua:**

- Karibu
- Hadithi ya uhitaji
- Song

Somo kuu
Shughuli (hiari)
Suluhisho la

**Vitabu vya kusoma**

- Mstari wa akati
- Shughuli

Maswali na Majibu ya (wanafunzi wa kale)
Mchezo (hiari)
Mahudhurio
Kazi

Ili wanafunzi wako watumie mafundisho haya katika maisha yao, wanahitaji sio tu umakinifu darasani lakini pia motisha. Wengi hujaribu kuwapa motisha kwa kutumia pipi na zawadi au kuwaadhibu ikiwa hawana umakinifu. Ingawa mbinu hizi mbili zinawafanya wawe na tabia njema darasani, hazitoi motisha wowote kwao KUISHI kulingana na kanuni walizosoma wanaporudi nyumbani. Sisi kama walimu wa watoto katika makanisa ya Kikristo, kazi yetu sio kutumbuiza watoto ili wasiwasumbue watu wazima. Badala yake, kazi yetu ni kukuza kizazi kipya cha waumini wanaomfuata, wanaomjua na wanaomtumikia Mungu. Ingawa kazi hii ni ngumu kwa kila mmoja wetu, jambo la ajabu ni kwamba Mungu mwenyewe anajali kila mtoto zaidi kutuliko, na anatupa nguvu zake ili tuweze kuendelea na kutupa hekima yake ili tumpe motisha na kumhudumia kila mtoto.

Ili kukusaidia kuwapa motisha wanafunzi wako, tunatoa "Hadithi ya Uhitaji" mwanzoni mwa kila somo ili kuwasaidia wanafunzi WATAMBUE uhitaji wao kwa Mungu na KUTUMIA kile wanachojifunza katika maisha yao halisi ya nyumbani.Kila hadithi inajumuisha mmoja ya wahusika 5 wa uongo ambao tumeunda. Tafadhali jisikie huru kubadilisha majina yao. Wazo moja ni kuwaomba wafanyakazi wa kujitolea kuigiza hadithi kila wiki. Ikiwa hilo haliwezekani, basi unaweza kusoma tu hadithi kwa watoto kwa sauti ya juu. Unaweza kuwaomba watoto wachangie mawazo ya kutafuta suluhisho. Usiwaambie kama mawazo yao ni mabaya, mazuri, si sahihi, au ni sahihi, na usitoe suluhisho lolote bado. Tumia tatizo lililopo ili kuwafanya watoto kuwa makini zaidi na somo.

Sehemu ya Suluhisho inakuja baada ya somo. Ikiwa watoto walikuwa wameketi kwa muda mrefu, fanya shughuli kabla ya sehemu ya Suluhisho. Ukiwa tayari, wakumbushe watoto kuhusu Hadithi ya Uhitaji na kisha waigizaji wako watatokea ili kutoa suluhisho au kueleza suluhisho. Hii itasuluhisha changamoto kwenye sehemu ya hadithi ya uhitaji na kuwasaidia watoto kukabiliana na changamoto za shuleni na nyumbani.Kwa njia hii, utawapa watoto motisha wa kutumia mafundisho haya katika maisha yao ya kila siku!




## SOMO KUU

Mtaala huu ni muhtasari wa jumla wa Agano la Kale. Katika masomo mengi, tutaangazia maisha yote ya mtu fulani, au Shujaa, kwenye Biblia. Kama mwalimu, unaweza kutumia maelezo haya kupata uelewa na kusoma vifungu vya Bibilia vilivyoorodheshwa kabla ya darasa ili kupata ufahamu mpya. Muhtasari wa maisha ya kila shujaa umejumuishwa katika somo kuu. Jisikie huru kuwaomba watoto wachangie maelezo zaidi ya maisha ya shujaa ili kuchochea umakinifu wao.

Tafadhali hakikisha sehemu ya hadithi ni fupi, ili kuwa na muda wa kutosha wa kueleza jambo kuu: jinsi ya kutumia. Mwishoni mwa kila somo kuna nafasi ya watoto kufanya uamuzi. Uamuzi huu ndio jambo kuu katika somo nzima, ni kama kufunga mbao kwenye mchezo wa kandanda (soka). Katika kandanda hata ukicheza vizuri, upitishe mpira kwa wenzako na uzuie timu pinzani kupata mpira, lakini hufungi mbao, basi huwezi kushinda. Hakikisha unafika kwenye jambo kuu ili kuwasaidia watoto kulitumia katika maisha yao. Katika Yakobo 1:22-24 tunasoma, "Basi muwe watendaji wa neno na wala msiwe wasikilizaji tu, ambao wanajidanganya wenyewe. Tenda kile inachosema. Kwa maana kama mtu ni msikilizaji tu wa neno na wala hatekelezi alilosikia, atafanana na mtu ajitazamaye uso wake katika kioo, na baada ya kujiona alivyo, huenda zake na mara moja husahau anavyofanana." Katika 1 Wakorintho 10, tunasoma kwamba hadithi katika Agano la Kale ni mifano inayoonyesha tunachopaswa kufanya na kile hatupaswi kufanya. Kuangazia Mashujaa wa zamani ni kama kujiangalia kwenye kioo na hutupa fursa ya kujifunza kutoka kwa maisha yao. Hebu tuwafundishe watoto kufuata mifano ya mashujaa hawa na wajifunze kutokana na makosa yao na waishi kwa ajili ya Mungu.

## MSTARI WA WAKATI

Kila wiki wanafunzi wachore mstari katika ratiba kwenye vitabu vyao ili kuwakilisha maisha ya Shujaa wa Biblia. Kwa mfano, katika somo la 1, wanaangazia maisha ya Ehudi, katika mstari uliotiwa alama ya 1 kwa ajili ya somo 1. Kwa kutumia nambari zilizotolewa katika somo, wazo ni kwamba wanafunzi wanafaa kuhesabu mstari unafaa kuanzia wapi, na utakuwa na urefu wa kiasi gani. Kila mraba unawakilisha miaka 100. Kwa mfano, maisha ya Ehudi yanaanza 1300 kabla ya Yesu na yanaisha 4/5 ya mwaka wa 1200 kabla ya Yesu. Itakuwa ni jambo la kusisimua kuangazia maisha ya kila shujaa na maelezo ya kushangaza, kama ni ukweli kwamba waamuzi Debra na Gideoni waliishi katika wakati mmoja, nao Jephtha, Samsoni na Samueli waliishi katika kipindi sawa.



Ratiba ya matukio ya Agano la Kale

## KAZI

Kifaa kingine cha kuwasaidia watoto kutumia mafundisho ni kuwapa kazi ya nyumbani ya kila wiki. Kila somo lina shughuli ambayo watoto wanaweza kufanya katikati ya wiki.

Katika Yohana 14:23, Yesu alisema, "Mtu akinipenda atashika mafundisho yangu.na Baba yangu atampenda, nasi tutafanya makao yetu kwake."

Kwa kazi hizi, watoto wanaweza kutenda maishani yao kulingana na Mungu katikati ya wiki, sio tu kanisani. Kwa wanafunzi wakubwa pia kuna kazi ya kusoma Biblia. Chukua dakika chache darasani ili kujadili kazi ya nyumbani na kuwapa fursa ya kufanya mazoezi katika darasa. Toa thawabu kwa wale wanaomaliza kazi ya wiki iliyopita kwa pipi ndogo au zawadi.

## MAHUDHURIO / MCHEZO WA MASHUJAA




Nyenzo hii inakuja na seti ya kadi ili kuwapa watoto watakaohudhuria kila wiki. Hizi zinaweza kuwa kadi au stika za mahudhurio. Hata hivyo, inaweza pia kuwa mchezo! Mwishoni mwa kitengo (baada ya masomo 13, au miezi 3), watoto wanaweza kutumia kadi hizi ili kucheza mchezo.Soma maagizo ya mchezo kwa maelezo zaidi.

## MCHEZO MBADALA

Fanya watoto waandike namba 1 hadi 10 kwenye kipande cha karatasi.Kisha mwalimu anauliza maswali yoyote kati ya 10 iliyotolewa kutoka kwa maelekezo ya mchezo. Usitaje sifa katika mabano. Kwa kila swali, wanafunzi wanaandika ubora au sifa zinazohitajika katika hali hiyo: Nguvu, Uadilifu, Utiifu, Unyenyekevu, Huruma au Imani. Atakayepata majibu mengi sahihi anashinda pipi ndogo au zawadi.

# 1. MUNGU HUJIBU MAOMBI



**Hadithi ya Biblia: Ehudi**
Waamuzi 3:12-30

## FUNGU LA 1 LA KUMBUKUMBU

"Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu."
Wafilipi 4:6

## HADITHI YA 1 YA UHITAJI



Buzz alikuwa akihisi vibaya karibia mwaka mmoja, kwa sababu hata ingawaje alikuwa hapendi, hangeweza kuacha kutizama filamu katika televisheni ambazo zilionyesha vitu ambavyo hakufaa kutizama, na alijua. Kila mara alisema "Sitazitazama kwa sababu sifai kufanya hivyo, haimpendezi Mungu." Na kila siku hata bila kujua, aliketi hapo kama mtumwa wa televisheni, hadi siku moja akaelewa kwamba hawezi kukoma kwa kutegemea uwezo wake pekee. Akaanza kuomba kwa bidii.

## SOMO KUU LA 1

Karibu tena katika Shule ya Jumapili ya Mashujaa wa Imani. Tumekuwa tukiangazia watu muhimu katika Agano la Kale, na kuona ni vipi waliingiliana na Mungu na jinsi Mungu aliwasaidia katika maisha yao. Tunapoona vitu hivi, tunapokea himizo katika maisha yetu pia. Leo tutaangazia hadithi moja ya kushangaza mno katika Biblia. Baada ya wanaisraeli kuingia katika nchi ya ahadi chini ya Joshua, walitengeneza makao na kupanda mimea, na wakaishi pale kwa muda mrefu. Katika wakati huu, walimsahau Mungu na kuabudu viti vingine ambavyo si Mungu wa kweli! Wewe na mimi ni wenye dhambi, pia, na ingawaje tunajaribu juu chini kufanya kinachofaa, mara nyingine tunafanya makosa. Ili kuwapa adhabu, Mungu alileta majirani wao, Wamoabi, wakateka Israeli na kuwatesa kwa mika 18! Huo ni muda mrefu. Mara nyingine, inachukua muda mrefu kutambua adhabu ya mungu maishani mwetu.

Tunapomkubali Yesu Kristo, tunaingia katika familia ya Mungu, na tunakuwa wana wa Mungu, na hakuna kinachoweza kubadili jambo hili. Kama baba yeyote mzuri, Mungu atatuadhibu na kutufunza jinsi ya Kumfuata. Pia kuna matokeo kwa kila uamuzi tunaofanya maishani mwetu. Wanaisraeli walipogundua kwamba walikuwa matatani kwa makosa yao, walimwomba Mungu kuwaokoa. Tunaweza kumwomba Mungu kutusaidia katika hali ngumu pia. Halafu tunafaa kuamini kwamba Mungu atatusaidia, ila mara nyingine si kwa njia tunazotaka sisi. Huenda Wanaisraeli waliamini Mungu atachagua shujaa mmoja atakayewaleta pamoja na kuunda kikosi kikubwa na kushambulia nchi iliyokuwa ikiwakandamiza. Mungu hakufanya hivyo. Badala yake Mungu alimtumia Ehudi aliyetumia mkono wa kushoto, aliyejifanya alikuwa na habari za siri kwa mfalme wa Moabu, na kisha akamuua ndani ya Kasri lake. Baada ya hili, kweli aliwaleta wanaisraeli pamoja, lakini badala yake walingoja katika mto na kumwangamiza mwanamoabi yeyote aliyepita pale. Kama Mungu alivyookoa Israeli kwa kumtumia mtu mmoja aliyeitwa Ehudi, kwa njia ambayo hawakutarajiwa, Mungu aliuokoa ulimwengu kupitia Mwanawe Yesu, kwa njia ambayo haikutarajiwa. Wanaisraeli walidhani mfalme angekuja na kuwaokoa lakini badala yake Yesu ndiye aliyekuja na kufa kwa ajili yetu, kisha akafufuka ili kila anayemwamini aweze kuokolewa. Wakati mwingine unapokuwa katika shida ama katika hali ngumu,

kama rafiki yetu Buzz na televisheni, kumbuka kwamba Mungu anajibu maombi. Omba Mungu msaada na usubiri kuona Mungu akitumia usiotarajia kukusaidia.

Katika hali ngumu, nitaomba usaidizi kutoka kwa Mungu!


## SULUHISHO LA 1



Siku moja baada ya kuomba, majirani wapya walikuja kuishi karibu nao, na muda mfupi akawa marafiki nao na alienda kucheza nao kila adhuhuri. Ilikuwa ni jambo la kusisimua kwake. Baada ya wiki moja, akagundua badala ya kutizama televisheni, alikuwa kila mara akicheza na hakuwa na muda wa kuitizama. Kisha alimshukuru Mungu na kujihisi huru, kwani hakuhitaji kuitizama televisheni.

## SHUGHULI YA 1

**Kuku Kipofu**



Katika shughuli hii, chagua msichana au mvulana atakayejiziba macho kwa kitambaa. Watoto wengine watatengeza mduara, aliyejiziba atawekwa ndani ya mduara. Hakuna mchezaji anayeruhusiwa kutoka nje ya eneo la mchezo. Mtoto aliyejiziba macho atajaribu kuwagusa wengine na kwa kutumia mguso, atajaribu kujua ni nani. Unaweza kutenganisha wavulana na wasichana, wachezee mahali tofauti.

## MSTARI WA 1 WA WAKATI

Kwa kutumia maelezo katika maswali haya, watoto wanaweza kuchora ratiba ya matukio kwa Ehudi. Je, Ehudi alianza kuongoza Israeli lini? A. Hatujui kwa uhakika, lakini inakisiwa alianza mwaka wa 1297 Kabla ya Yesu.

Je, Ehudi aliongoza Israeli kwa muda gani? A. Miaka 80.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 1



| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | B | U | B | A | I | D | I | A | S | A |
| U | A | M | I | N | I | F | U | W | K | K |
| M | I | U | I | D | A | A | B | U | D | U |
| A | J | B | H | B | A | S | O | M | H | O |
| N | O | A | M | S | I | K | A | A | S | K |
| A | S | O | D | A | O | W | T | H | H | O |
| S | H | M | I | L | H | Y | I | D | A | L |
| N | U | A | E | H | U | D | I | I | N | E |
| I | A | W | A | M | A | U | G | N | U | M |
| M | A | T | O | K | E | O | Y | O | S | A |



## MASWALI NA MAJIBU YA 1

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, Mungu akitaka nifanye kitu cha ujasari kama Ehudi, je, kama nahisi woga? Je, ni kawaida kuhisi woga? (Kuwa na ujasiri sio kutokuwa na woga, bali ni kusonga mbele hata unapohisi woga.)
2. Je, ni adhabu gani umewahi kupata kwa sababu ya makosa yako? (Himiza wanafunzi kujadiliana kuhusu adhabu tofauti na wakati ambapo ni sisi wakulaumiwa na wakati ambapo sio sisi wakulaumiwa.)
3. Je, vita ni kitu kizuri? (Jadiliana tofauti kati ya kumuua mtu, na kuwa kwenye vita halafu unamuua mtu. Wacha washiriki mawazo yao tofauti kuhusu vita katika ulimwengu, na usisahau kuzungumzia vita vinavyoendelea siku hizi.)

## MCHEZO WA 1

**Kumlilia Mungu**



Watenganishe wasichana na wavulana wachezee mahali tofauti. Watoto wasimame katika mstari na kushikana mikono. Halafu watoto walio katika kila mwisho wapite chini ya mikono au juu ya mikono hadi wachanganyike kabisa. Baada ya hili, wataanza kumlilia Mungu, wakimwita kwa sauti kubwa "Mungu Tusaidie". Halafu mtoto mmoja atakuja na kuwasidia kutoka katika mchanganyiko huo.




## MAHUDHURIO YA 1

Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Ombi**

## KAZI YA 1 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kazi ya ziada wiki hii ni kuomba Mungu ndani ya darasa lako (shule) kuhusu wakati Fulani mgumu unaopitia, pamoja na mwanafunzi mwenzako au na mwalimu. Usifunge macho, ama kusema kwa sauti ya juu, kwa sababu Mungu anayaskia mawazo na roho yako. Omba kuhusu kitu mahususi na kinachowezekana na usubiri jibu la Mungu.

**Soma**

Siku ya 1: Waamuzi 4:1-5
Siku ya 2: 4:6-10
Siku ya 3: 4:11-14
Siku ya 4: 4:15-20
Siku ya 5: 4:21-24

# 2.MUNGU NI MWENYE HAKI



**Hadithi yaa Biblia: Debora**
Waamuzi 4:1-24, 2:24-27

## FUNGU LA 2 LA KUMBUKUMBU

"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao." Waebrania 11:6

## HADITHI YA 2 YA UHITAJI



Siku moja katika kanisa la Comet, mwalimu wa Shule ya jumapili hangeweza kuwasili kwa sababu alikuwa mgonjwa. Aliongea na Comet na kumwomba awahudumie watoto siku hiyo. Alifaa kuhakikisha hawakutoka darasani, halafu acheze filamu ya Biblia. Mwanzo, Comet hakukubali. Alifikiria "Itakuwa vizuri nikikaa hapa darasani nikisikiza tu." Mwalimu alipoona Comet hajakubali, alimwambia "Tafadhali". Comet alikubali, lakini aliomba mtu mwingine awahudumie watoto na kisha yeye angesaidia.

## SOMO KUU LA 2

Karibu tena kwa Mashujaa wa Imani! Wakati uliopita, tulisoma jinsi Mungu aliweza kuokoa Israeli kwa njia ambayo hawakutarajia kwa kutumia mtu aliyeitwa Ehudi. Wakati huu tutaona kwamba Mungu ni wa Haki. Kwa mara nyingine wanaisraeli walifanya dhambi, na mfalme Jabini wa Kanani aliwakandamiza kwa kutumia Sisera, kamanda wa jeshi lake. Wakati huo kulikuwa na nabii aliyeitwa Debra, aliyewaongoza wanaisraeli akiwa chini ya mnazi. Nabii ni mtu anyezungumza maneno ya Mungu, na hata ingawaje kwa kutumia Debra Mungu alimwita mwanamme mmoja aliyeitwa Baraki, kuwaleta pamoja wanaisraeli na kuwashambulia wanajeshi wa Sisera. Wiki iliyopita tulijifunza jinsi ya kumwomba Mungu msaada tunapokuwa matatani. Mara nyingine, ni watu wengine wanaohitaji usaidizi na Mungu anatuita kufanya jambo ili kuwasaidia, kama Comet katika hadithi ya leo. Je, Mungu atakapokuita, jibu lako litakuwa gani? Baraki alimwambia Debra kwamba angeenda vitani iwapo angeandamana naye. Tunapoingiwa na hofu, tunajaribiwa kuweka imani yetu kwa watu tunaowaona badala ya kuiweka kwa Mungu ambaye hatumuoni. Tunaweza kusahau jinsi Mungu ni mkuu. Mungu ni mkuu kwamba aliumba ulimwengu wote! Aliumba nyota ambazo ni kubwa sana hata hatuwezi kuzifikiria na ziko mbali sana hata hatuwezi kuziona. Aliumba bahari, anga kubwa, mawingu yaning'inie, akaumba milima yote mikubwa.Yeye ndiye anayeongoza ulimwengu mzima, anaongoza mataifa, amekuwa akiandika historia, na anajua kila kitu kuhusu yajayo. Angalia anga au uwaze kuhusu anga na ukumbuke yeye ni mkuu. Anapokuita, unafaa kuamini kwamba atakusaidia kufanya lolote analokuita kufanya. Kila unapoingiwa na hofu kwamba unalotaka kufanya ni la kutia hofu, fikiria anga, nyota, na milima na ukumbuke kwamba Mungu ni mkuu kuliko lolote linalokutia hofu. Kwa sababu Baraki hakumwamini Mungu alimwamini Debra, Mungu alifanya mwanamke mwingine kupata fahari ya kumwua Sisera. Baraki na wanaisraeli walishinda vitani kwa sababu Mungu alikuwa nao. Sisera alikimbia na kujificha katika hema ya mwanamke aliyemwamini na kulala kwa uchovu. Alipokuwa amelala, mwanamke Yule alimwua, na

Wanaisraeli walipoimba nyimbo za kutukuza, walimsifu mwanamke yule badala ya kumsifu Baraki. Mungu ni mwenye haki, na Yesu alisema kwamba atatutuza kulingana na matendo yetu. Tunaweza kupokea baadhi ya tuzo hapa ulimwenguni, na zingine Mbinguni. Kwa hali yoyote, tunaweza kuamini kwamba Mungu atatupa tuzo, kwa kuwa mashujaa kwa ajili yake.

Natambua kwamba Mungu ni wa haki na atanituza kulingana na kila ninachofanya katika maisha.

## SULUHISHO LA 2



Mhubiri wa kanisa alikuwa ametayarisha zawadi ndogo kwa Comet. Alikuwa ampe zawadi ndogo ya pesa kwa usaidizi wake. Mhububiri alipogundua kwamba watu wawili walihusika katika kuhudumia darasa, ilimbidi kugawanya pesa zile mara mbili. Baada ya kila kitu, Comet, aligundua kwamba hakuhitaji usaidizi wowote.

## SHUGHULI YA 2

**Mahakama ya haki**

Watoto wataketi katika mviringo; Mwalimu ataunda hali kama mfano, (Baba Fulani amewanunulia watoto wake vipungu lakini kwa hali kwamba ni lazima wagawane. Msichana anaamua kuvificha kutoka kwa kakake, ndio asiweze kuvitumia kwa sababu miguu yake inanuka vibaya. Ni haki ama si haki?) Mtoto aliyeketi upande wa kulia atakuwa kama mwamuzi na atasema kama hali hii ni ya haki ama si ya haki. Lakini kabla ya hayo, wanafunzi hao wengine watakuwa waamuzi.

Kwanza wale ambao wanaamini jambo hili ni la haki watainua mikono. Kisha watahesabiwa.




Baadaye wale wanaoamini jambo hili si la haki pia watainua mikono yao, na kuhesabiwa. Halafu baadaye, Jaji, atafanya uamuzi wa mwisho kwa kutangaza iwapo jambo hili ni la HAKI AU SI LA HAKI. Halafu mtoto mwingine atakuwa jaji, kufanya uamuzi kuhusu nini ni haki.

## MSTARI WA 2 WA WAKATI

Nani aliongoza Israeli baada ya Ehudi? A. Debora.
Je, Debora aliongoza kwa miaka mingapi? A. Miaka 40.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 2





| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | N | Y | H | B | A | R | A | K | I | F |
| I | J | A | S | A | Y | N | A | Y | N | U |
| W | K | S | H | R | D | S | A | R | A | F |
| I | O | I | U | A | R | E | S | I | S | I |
| I | I | G | J | K | D | U | B | I | J | N |
| B | N | W | A | A | J | I | I | O | W | I |
| A | I | D | A | W | A | Z | H | J | R | M |
| N | M | J | I | L | E | A | R | S | I | A |
| S | A | I | L | B | I | B | T | U | A | W |
| N | G | O | M | B | E | U | G | N | U | M |

## MASWALI NA MAJIBU YA 2


**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, ni vitu gani huwa tunafanya kila siku na Mungu anaviona? Je, atatuzawadi? (Mwalimu, ni wazo nzuri kujifanya kwamba hauamini kwamba Mungu anaona kila kitu na uzungumzie kuhusu mambo yoye ili kujua maoni yao. Kwa mfano, nikitizama runinga, Mungu hanioni, nk. Mwishowe, hitimisha kwa kusema kwamba Mungu huwa anaona kila kitu. Jambo hili litayafungua macho ya wanafunzi wako.)
2. Nahisi tu kuitizama televisheni. Ni sawa? Mbona nisifanye hivyo? (Vitu vingine sio makosa kimaadili, lakini ni kuupoteza wakati. Sisi sote tunahitaji kumpumzika kila siku. Lakini jaribu kuzungumza na wanafunzi wako kuhusu idadi ya saa wanazotumia kucheza michezo ya video au kutizama televisheni, ndio waelewe wanaupoteza muda mwingi sana. Kama Mungu hutuzawadi kwa kila kitu, si basi itakuwa ni vizuri kutenda vitu vingine vizuri?)
3. Mbinguni kutakuwa aje? (Kila mtu ana maoni tofauti kuhusu mbinguni. Wakati mwingien, watu kwenye ulimwengu hutuambia kwamba mbinguni hakutakuwa na mambo ya kufanya, ambapo tutaelea tu juu ya mawingu bila chochote cha kufanya. Lakini Yule aliyeumba ulimwengu huu, ndiye atakayeumba mbingu nyingine na ulimwengu wa toleo la 2.0, ambao utakuwa umejaa uzuri bila


chochote kibaya. Biblia inatumbia kwamba kutakuwa KUZURI zaidi ya tunayoamini. Chukua muda mfupi pamoja wanafunzi wako ili kuwaza mambo mazuri zaidi na kuhusu ZAWADI KUBWA. Waulize, wanaweza kufanya nini ili kushinda kompyuta kibao mpya ama simu inayowavutia zaidi? Je, Mungu atakuwa na zawadi kama hizi mbinguni?

## MCHEZO WA 2

**Kuchora bila kuona.**



Gawanya wanaoshiriki katika vikundi. Waombe waketi bila kuangaliana. Mpe mtoto mmoja kati ya wawili kalamu na karatasi na huyo mwingine mpe picha. Yule aliye na picha atamueleza mwenzake kuihusu picha bila kumwambia kilicho halisi kwenye picha. Kwa mfano, iwapo picha ni wadudu kwenye tofaa, hauwezi kusema, “Chora tofaa lenye wadudu ndani yake”. Unaweza kusema, “Chora mchirizo kwenye upande wa kushoto.”  Aliye na kalamu na karatasi atachora anachodhani kinawakilisha maelezo aliyopewa. Weka muda wa kikomo kuwa dakika 10-15.




## MAHUDHURIO YA 2

Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Debora**

## KAZI YA 2 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kazi ya ziada wiki hii, ni kuchagua shughuli Fulani kama vile kuzungumzaa kumhusu Yesu Kristo, kumpa moyo mtu, ama kuwasaidia wazazi wako nyumbani, ambapo utachukua jukumu la kufanya hivyo kila siku. Inaweza kuwa nyumbani au shuleni. Isitoshe, unaweza kujitolea kuwa utakuwa unafanya Fulani kanisani. Iwapo unaogopa, tizama juu kwenye nyota ama mawingu, na uwaze kuhusu ukuu wa Mungu wetu aliyeziumba.

**Soma**

Siku ya 1: Waamuzi 6:1-13
Siku ya 2: 6:14-26
Siku ya 3: 6:27-40
Siku ya 4: 7:1-15
Siku ya 5: 7:16-25

# 3. MUNGU ANATHIBITISHA NENO LAKE



**Hadithi ya Biblia: Gideoni**
Waamuzi 6:1-7:25

## FUNGU LA 3 LA KUMBUKUMBU

"Bali wao wamngojeao BWANA watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mbawa kama tai; watapiga mbio, wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu, wala hawatazimia." Isaya 40:31

## HADITHI YA 3 YA UHITAJI



Kakake Buzz ni kijana. Siku moja alikuwa akiomba na kusoma Biblia, kisha Mungu alimwambia…

Kwamba Mungu angemtumia katika kikundi cha kuabudu kanisani mwake! Alishtuka sana kwa sababu hata hakujua kucheza sanaa yoyote ya mziki, hivyo hakuamini, na alidhani alikosea.

Halafu alimwomba Mungu na kuumuliza kama hivyo ndivyo Mungu angependa…

## SOMO KUU LA 3

Wiki iliyopita, tuliona jinsi Baraki alivyoweka imani yake kwa watu badala ya Mungu. Wiki hii tutasoma kuhusu mtu anayeitwa Gideoni. Kwa mara nyingine, Wanaisraeli walifanya dhambi, na wanamidiani waliwadhulumu kwa kiasi kikubwa kwamba walikosa vyakula ua wanyama. Iliwabidi kupika vyakula kwa siri. Kila mtu ajifanye kula kwa siri. Siku moja Malaika alikuja na kumwongelesha Gideoni, na kumwambia kwamba Mungu angemtumia kuokoa Israeli. Alimwambia Gideoni akwende kwa nguvu alizokuwa nazo. Gedioni alishangaa kwani alijiona mwenye uwezo mdogo sana. Je, ushawahi kufikiria "Mimi ni mtoto mchanga! Je naweza kufanya nini? " lakini Mungu anaweza kutumia uwezo mdogo ulio nao na kukuwezesha kufanya jambo kubwa. Mungu ni mwenye nguvu zote na hivyo hahitaji usaidizi wa binadamu yeyote mwenye nguvu. Gedioni aliomba kitu ambacho sisi wote tunaweza kuomba: aliomba hakikisho, kama alivyofanya Buzz katika hadithi ya leo. Mungu anapendekeza tumuombe kuhakikisha neno lake halafu tulifuate. Kinachomkasirisha Mungu ni kuasi na kukosa imani. Gideoni alipogundua alikuwa akizungumza na Malaika alishtuka sana. Mungu alimwambia, "Amani! Usiingiwe na hofu." Yesu alitwambia kwamba anatupa amani yake na kwamba yupo nasi kila wakati na anatwambia mara kwa mara kwamba hatufai kuogopa. Tunapokuwa na imani, Tunajua Mungu yupo nasi, na anapotuhakikishia neno lake, basi tunatia imani yetu mikononi mwake na kumtii. Gideoni aliharibu madhabahu ya miungu ya sanamu katika mji wake, na kisha akajenga madhabahu ya Mungu wa ukweli. Halafu Mungu akamwelekeza kukusanya wanaisraeli ili kupigana na jeshi KUBWA la Wanamidiani, Kwa mara nyingine, Gedioni alimwomba Mungu kutoa hakikisho kuhusu neno lake, na kuomba jambo ambalo halingewezekana. Aliweka kipande cha ngozi kwenye ardhi. Asubuhi, ngozi ile ilikuwa imeloa maji, lakini ardhi iliyoizunguka ilikuwa imekauka. Gideoni aliwakusanya Wanaisraeli 32,000, lakini Mungu haangazii nguvu yetu, anaweza kutumia kitu kidogo sana. Alimwamurisha Gideoni kuwatuma watu nyumbani hadi

wakabaki wanaume 300. Funga macho yako na ufikirie wanaume 300 dhidi ya jeshi kubwa. Mungu, kwa mara nyingine alihakikisha neno lake. Alimwamurisha Gideoni kwenda chakubimbi hadi kambi ya adui, ambapo alimsikia mtu akizungumza kuhusu ndoto yake ambapo aliona Gideoni akiwashinda. Ukiona kwamba Mungu yupo nawe, fanya alivyofanya Gideoni,na umwabudu Mungu. Gideoni aliwapa wanaume wale 300, mataa, vyungu na tarumbeta. Katikati mwa usiku, walizingira jeshi lile. Halafu kwa pamoja walivunja vyungu vile, ili kumulika na mataa, kupuliza tarumbeta halafu wakapiga unyende. Jeshi lote lilikimbia kwa mshtuko. Israeli walishinda vita hivyo kwa rahisi, kwa sababu Mungu alikuwa nao. Mungu anapokuita kumbuka ni mwenye Nguvu. Mwulize akupe hakikisho, halafu ufanye analokuita kufanya.

Naweza kumwomba Mungu kuhakikisha neno lake kwangu. Nitamtii.

## SULUHISHO LA 3



Miezi kadhaa baadaye katika Kanisa, mhubiri alimwongelesha kwa ajili ya Mungu na kumwambia kile alichomwambia hapo awali. Hapo ndipo aligundua kuhakikishwa kwa neno la Mungu, na kisha akaanza kujitayarisha katika muziki.

## SHUGHULI YA 3

**Shajara**



• Tengeneza shajara au kijitabu chenye vijikaratasi.


• Waambie kila siku wataandika ushuhuda ili kuhakikisha uwepo wa Mungu. Itakuwa ni jambo lililowafanyikia au jambo watakalo-ona ambalo linahakikisha uwepo wa Mungu.

## MSTARI WA 3 WA WAKATI

Je, Gideoni alizaliwa mwaka upi? Hatujui kwa hakika, Lakini inakisiwa alizaliwa mwaka wa 1252 kabla ya Yesu. Je, Gideoni alifariki lini? Hatujui kwa uhakika, lakini inakisiwa alifariki mwaka wa 1152 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 3






| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| N | U | F | I | A | H | D | T | V | U | Y |
| I | J | B | M | A | D | H | A | I | E | I |
| I | N | O | E | D | I | G | R | N | A | N |
| T | N | G | U | H | U | B | Y | A | K | A |
| K | A | V | U | D | E | E | M | M | I | I |
| W | A | M | U | I | N | H | B | A | A | D |
| B | T | B | F | G | V | U | D | A | L | I |
| T | A | R | U | M | B | E | T | A | A | M |
| K | M | V | S | M | A | T | A | J | M | A |
| A | U | L | O | W | A | D | I | N | A | W |
| O | H | S | I | T | I | B | I | H | T | U |


## MASWALI NA MAJIBU YA 3

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**


1. Itakuwaje Mungu akiniambia HAPANA? (Hili linatendekea sisi sote, wakati kuna kitu tunachotaka SANA, hivyo tunapohisi HAPANA, tunamuuliza Mungu kutapu uthibitisho mara kadhaa. Mungu ni mwenye subira na sisi, lakini tunafaa kukubali jibu la HAPANA Na kumtii.)
2. Je, Mungu huwa ananikasirikia? Mbona? (Je, ni katika hali gani Mungu anaweza kukasirika? Tunapokosa kutii na kudanyanganya ili kuficha kitu, tunapokosa kuamini kufanya jambo lingine, ama kuteta sana kwamba hatuwezi kulifanya. Mungu hakasiriki tunapojawa na woga na kumuuliza adhibitishe neno lake.)
3. Je, Mungu anataka kuzungumza nami? (Jadiliana kuhusu mada hii, Mungu atasema nini, Je, Mungu anataka kuzungumza na nani Anapoongea. Hitimisha kwamba huwa anazumngumza na kila mmoja wetu, kila siku, na kuhusu chochote.)

## MCHEZO WA 3

**Kisia ni Nani**



Tengeneza timu mbili. Katika timu moja, kila mtoto anawakilisha mtu fulani katika masomo ya hapo awali, jukumu hili litatolewa kwa siri na mwalimu. Timu ile nyingine itajaribu kujua wanawakilisha kina nani. Wanaweza kuuliza maswali mahsusi na wanaojibu watafanya hivyo kwa jibu rahisi la Kweli au La. Hakuna anayefaa kudanganya. Kwa mfano, kama mshiriki ni Musa na swali ni "Je, Ulitengeneza safina?" jibu litakuwa, La." Jina lako ni nani?" swali la moja kwa moja kama hili, haliruhusiwi. Timu inayohusika katika kuuliza maswali wanaweza kusema wanayemfikiria iwapo wanayemfikiria ndiye. Wakimaliza, waambie wabadilishane majukumu, wachanganye, na kisha wacheze tena.




## MAHUDHURIO YA 3

Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Gideoni**

## KAZI YA 3 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kazi ya ziada wiki hii ni kutafuta kitu ambacho kinathibitisha uwepo wa Mungu, kitu kitakachotendeka au kitu utakachokiona maishani mwako au ya mtu mwingine. Andika kuhusu kitu hicho au uchore picha katika kitabu chako nyumbani, alafu umwambie mwalimu wako kanisani kuhusu kitu hicho.

**Soma**

Siku ya 1: Waamuzi 10:6-14
Siku ya 2: 10:15-11:3
Siku ya 3: 11:4-13
Siku ya 4: 11:28-34
Siku ya 5: 11:35-40

# 4.MUNGU ANAKUDHAMINI



**Haditi ya Biblia: Yeftha**
Waamuzi 10:6-11:13, 11:29-40

## FUNGU LA 4 LA KUMBUKUMBU

"Tazama, Mungu ni hodari, wala hamdharau mtu ye yote; Ana uweza katika nguvu za fahamu." Kazi 36:5

## HADITHI YA 4 YA UHITAJI



Taffy alihisi vibaya sana kila siku shuleni. Kila mtu shuleni alimcheka kwa sababu ya familia yake au kwa sababu yeye ni Mkiristo. Aliketi peke yake wakati wa chakula cha mchana. Hakujua kucheza mpira vizuri, hivyo katika somo la mazoezi, wakati watoto wengine wakichaguliwa katika timu, yeye kila mara alichaguliwa wa mwisho. Angewaambia wanafunzi wengine karibu naye jinsi walivyojua kuucheza mpira, lakini walimcheka jinsi yeye hakujua kucheza. Mara nyingi, walimpuuza. Wiki moja alijihisi mgonjwa na hangeweza kwenda shuleni. Lakini alipojihisi vizuri, aliogopa kurudi shuleni kutishwa. Aliomba, "Mungu Baba, Nakuomba unisaidie!"

## SOMO KUU LA 4

Karibu tena kwenye Mashujaa wa Imani. Leo tutasoma kuhusu anachokienzi Mungu. Fikiria kwa muda mfupi kuhusu vitu tofauti watu wanavyoenzi, vitu tofauti ambavyo vinaonyesha hadhi ya mtu katika maisha. Je, ni vitu gani watu wanavyosema vinafanya mtu kuwa mwenye umuhimu? (Kubali majibu tofauti) Ulimwengu unatwambia kila wakati kuangalia utajiri, uwezo (kama hadithi ya Taffy katika hadithi ya leo), vipaji, familia, rangi ya ngozi, nywele, nguo, hata meno yasiyo na hila! Ulimwengu unawaenzi watu kwa njia tofauti kulingana na vitu hivyo, na kuwapa hadhi ya juu watu wengine na wengine ya chini. Lakini Mungu haangalii mambo haya. Je, unafikiria Mungu anaangalia nini? (Wakubalishe watoto kufikiria, lakini bado usiwape jibu.) Wacha tuangazie hadithi ya leo kutoka kwenye Biblia.

Kwa mara nyingine, wanaisraeli walifanya dhambi kwa kuabudu miungu mingine badala ya Mungu wa ukweli. Halafu Wafilisti na Waamoni wakawadhulumu kwa miaka 18. Walimwomba Mungu awaokoe, na wakaharibu miungu yote ya sanamu. Mungu alijibu maombi yao na akamtuma mtu kwenda kuwaokoa. Je, ni mtu wa aina gani ambaye angeweza kuikomboa Israeli? Ungeweza kufikiri angekuwa ni shujaa mwenye hadhi ya juu, na aliyependwa na kuheshimiwa na watu wote… lakini Mungu alimchagua mtu aliyeitwa Jephta, mwana wa kahaba. Ulimwengu ulidhani hakuwa na umuhimu wowote, walimdharau, na ndugu zake hata walimfukuza kwa sababu ya tabia za mamake. Haikuwa ni matendo ya haki. Alinyanyaswa kwa tendo ambalo yeye mwenyewe hakulitenda! Yesu Kristo pia aliyapitia haya. Viongozi wa Wayahudi walimdhihaki, wakamtukana, na kumuua Yesu hata kama hakufanya kosa lolote. Je, Mungu anatazama jambo hili vipi? Biblia inatwambia Mungu haangalii tunavyokaa kimwili kama ulimwengu unavyotutizama. Mungu anaangalia Roho zetu (1 Samweli 16:7). Yesu alisema kuwa haina maana kupata vitu vyote ulimwenguni (Hadhi, Utajiri, umuhimu na kadhalika) na kisha kuupoteza uhai

wako. (Mathayo 16:26) Chunguza roho yako. Uhai wako una umuhimu kuliko ulimwengu mzima! Yesu alipofariki, alifanya hivyo kwa ajili yako kwa sababu anakudhamini. Hakuna hadhi yoyote ulimwenguni ambayo inaweza kutoa au kuongeza jinsi Mungu anakudhamini. Mtizame mtu aliye upande wako wa kushoto na wa kulia. Kila unayemwona pia ana umuhimu kuliko ulimwengu mzima. Katika hadithi ya hivi leo, Mungu alibadilisha nyoyo za watu. Walipokuwa kwenye shida, walikwenda kwa Jephta ambaye walikuwa wamemfukuza na kumwomba msaada. Aliwaoongoza Wanaisreali kwa ushindi na akawa kiongozi wa Israeli kwa miaka 6.

Najua maoni ya Mungu ndio yenye umuhimu mkubwa. Najua kwamba Mungu ananidhamini.

## SULUHISHO LA 4



Taffy alipokwenda shuleni, alipigwa na mshangao. Watoto wengine walionekana kufurahia kwamba amerudi shuleni! “Tulitaka sana kukuona! “Walisema“ Hatuna msisimuko bila wewe. Kila wakati unatutia moyo.” Halafu wakati wa somo la mazoezi hakuchaguliwa akiwa wa mwisho tena, hata ingawaje bado hakujua kucheza vizuri.

## SHUGHULI YA 4

**Chora mkono wako**



Waulize watoto wachore mikono yao katika karatasi la A-4 au katika vitabu vyao. Katika kila kidole, waandike kitu ambacho wangependa Mungu awape, kwa mfano zawadi au ombi kutoka kwa mtu mwingine.

## MSTARI WA 4 WA WAKATI


Je, Jephta alizaliwa mwaka gani? Hatujui kwa uhakika, lakini inakisiwa ni mwaka wa 1118 kabla ya Yesu. Je, Jephta alifariki lini? Hatujui kwa uhakika, lakini inakisiwa alifariki mwaka wa 1094 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 4



| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | I | M | D | A | H | T | F | E | Y |
| L | B | I | U | S | H | U | J | A | A |
| I | N | O | M | A | A | W | M | I | I |
| M | H | N | A | Y | E | U | A | L | M |
| U | P | E | N | D | O | S | A | B | W |
| M | I | K | A | H | I | H | D | I | A |
| G | W | A | S | A | A | I | I | B | M |
| U | G | N | U | M | F | N | L | D | U |
| U | P | O | S | A | I | D | I | A | Z |
| M | W | A | F | I | L | I | S | T | I |

Katika shughuli ya dhamana, kumbuka kwamba Mungu anazingatia kwamba uhai wa kila mtu una umuhimu kuliko ulimwengu mzima. (Mathayo 16:26), na haangalii tofauti baina ya watu. (Mathayo 22: 16, Wagalatia 3: 28). Jibu ni 10 au dhamana tosha kwa kila mtu.



## MASWALI NA MAJIBU YA 4


**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Ni kesi gani za ubaguzi ambazo umeshuhudia darasani mwako shuleni? (Anzisha majadiliano miongoni mwa wanafunzi kuhusi hali tofauti ambazo wameshuhudia, na jinsi ubaguzi ni mbaya na unavyoumiza anayebaguliwa.)
2. Ninapogundua ubaguzi, mbona nihusike? (Jadiliana ukweli kwamba hakuna kitu kibaya kama kuona uovu na kisha kutofanya an kutosema chochote wakati mtu anahitaji ulinzi wako.)
3. Mbona hawaachani na mimi? (Binadamu ni viumbe wa kijamii, na mara nyingine huwa tunajipata katika visa vya ubaguzi, hamu ya kutaka kuwa maarufu kuliko wengine, na tunajiingiza kwenye dhambi. Watu hawatawahi kutuacha na amani. Lazima tujifunze kujikinga na kuwakinga wengine. Tunaweza kuwa imara kwa kujua sisi ni nani ndani ya Yesu na kutojali wanachosema wengine.)

## MCHEZO 4


**Kudhaminiana**

Watoto washikane mikono na kuunda mduara. Unaweza kuwatenganisha wavulana na wasichana ili wacheze kando. Mtoto mmoja atakuwa nje ya mduara na atakimbia kuzunguka mduara huo. Atachagua mtoto kutoka mduara na kisha atakimbia upande mwingine ili asipoteze nafasi yake. Mwenye atafika pale mbele, ndiye mshindi. Mwenye ameshindwa basi atamsifu kwa sauti kubwa mwenye ameshinda kwa jambo fulani nzuri, Kwa mfano: Manuel ni mwerevu sana.



## MAHUDHURIO YA 4

Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Vitabu Vya Mashairi**



## KAZI YA 4 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kazi ya ziada wiki hii ni kujitathmini: Unajiona aje? Kuwa mwangalifu usije ukajilinganisha na wengine. Ukijihisi mwenye dhamani ya chini, kumbuka kwamba Mungu alikuumba jinsi ulivyo na anakudhamini na anakupenda. Kama unahisi mwenye dhamani, kumbuka kwamba uaminifu wako upo katika Yesu Kristo, na sio kwako mwenyewe. Kila siku wiki hii sema kwa sauti ya juu," Mimi ni wa Yesu, na ananidhamini na ananipenda."

**Soma**

Siku ya 1: Waamuzi 13:1-5
Siku ya 2: 15:9-16
Siku ya 3: 16:4-10
Siku ya 4: 16:15-22
Siku ya 5: 16:23-30

# 5.MAELEZO



**Hadithi ya Biblia: Samsoni**
Waamuzi 13:1-25, 14:5-6, 15:9-20, 16:2-31

## FUNGU LA 5 LA KUMBUKUMBU

"Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji." Waebrania 4:16

## HADITHI YA 5 YA UHITAJI



Asubuhi hii, wazazi wa Taffy walikwenda kazini, waliongea naye kwamba asisahau kuweka vyakula vilivyokuwa jikoni kwenye friji." Hivyo tu ndio tunataka ufanye, na uwe mtoto mzuri" Taffy alifikiria "Ni jambo la kushangaza kwamba sijawahi kuachiwa jukumu lolote. Hata hivyo, nitafanya nitakalo." Taffy alienda kusoma gazeti na akapanga kufanya jukumu alilowachiwa na wazazi wake baadaye, lakini akasoma gazeti sana na hivyo akasahau jukumu alilowachiwa.

## SOMO KUU LA 5

Karibu tena! Leo tutasoma kumhusu shujaa fulani asiye wa kawaida. Siku moja Malaika wa Mungu aliwatembelea wanandoa ambao hawakuwa na mwana, na akawaambia wangepata mtoto mvulana. Angekuwa mnadhiri, ambaye angejitolea kwa Mungu kwa ahadi zisizo za kawaida. Hakufaa kugusa kileo, wala mfu, wala kuikata nywele yake maisha yake yote. Ahadi hii ya Mnadhiri inaonyesha picha ya maisha yetu na Mungu, ila mambo haya hatuyafanyi siku hizi kwa sababu Yesu alitimiza amri. Lakini Mungu hajabadilika, na anachunguza kwa undani. Iwapo tu Samsoni angetimiza ahadi, Mungu angeendelea kumpa nguvu zisizo za kawaida. Siku moja alimshambuliwa na simba, na alimwua Yule simba kwa mikono yake mitupu! Wakati mwingine, Wanaisraeli walimpatiana kwa Wafilisti. Samsoni alikata kamba mpya zilizomfunga, akachukua mfupa, na kuwaua Wafilisti 1000 peke yake! Wakati mwingine, Wafilisti walizunguka mji wake. Samsoni aling'oa Milango ya mji na kuibeba hadi juu ya mlima. Hakuna kitu Wafilisti wangefanya ili kushinda nguvu ya Samsoni. Kwa njia hii, tunayo nguvu ya Mungu ndani yetu na adui yetu, shetani, hawezi kutushinda. Baadaye, Samsoni alipendana na mwanamke Mfilisti aliyeitwa Delila. Alimchezea shere hadi akamwambia siri ya nywele yake. Alipoikata nywele yake, nguvu zake ziliisha! Wafilisti walimnasa, wakamng'oa macho na kisha wakamtia kwenye jela. Mungu anaangalia maelezo mahususi. Katika maisha yetu, tunaweza kwenda kanisani na kukosa kumakinika. Inaweza kuwa ni kukosa kutii, kama hadithi ya Taffy hii leo, ama hata pingamizi dhidi ya wazazi wako ambayo umekuwa ukijaribu kuificha. Inaweza kuwa ni chuki na mtu mwingine. Chochote kile, hauwezi kumficha Mungu chochote. Unaweza kukitambua, ukatubu, na Mungu atakurudishia nguvu yako. Baada ya muda, nywele yake ilimea tena. Katika sherehe kubwa, Wafilisti walimleta Samsoni ili kumdhihaki. Akamwomba Mungu amrudishie nguvu yake mara ya mwisho, akasukuma majabali ya hekalu, na jumba lote likaporomoka. Aliwauwa Wafilisti wengi katika kifo chake kupita idadi aliyoua wakati wa maisha yake. Kwa njia kama hii, Yesu alitembea hapa ulimwenguni kwa nguvu za Mungu - hakuna yeyote ambaye angempinga. Hata ingawaje Samsoni alifanya makosa mengi, Yesu hakufanya dhambi hata mara moja.



WOW!

Kama Samsoni, Yesu alizishinda dhambi na shetani aliposurubiwa, akafa, na kufufuka tena. Kwa sababu ya Yesu, tunayo neema tunapokosea kama Samsoni. Yesu yupo nasi na atatufunza jinsi ya kuishi juu yake, na mara nyingi kumfuata kunamaanisha kumakinika zaidi.

Nitamakinika na kumfuata Mungu.




## SULUHISHO LA 5

Wazazi wake waliporudi, walileta wageni wakule. Kwa mshangao, vyakula ambavyo walikuwa wamepika vilikuwa vimeharibika.

## SHUGHULI YA 5

**Nafasi mpya**

Chora mstari kwa karatasi na kuugawanya mara mbili. Katika sehemu ya kwanza, utaandika hali ambapo mambo yalikwenda mrama. Katika sehemu nyingine utaandika jinsi Mungu anaweza kukupa uwezekano wa kubadilsha hali hizi.



## MSTARI WA 5 WA WAKATI

Je, Samsoni alizaliwa mwaka gani? Hatujui kwa uhakika, lakini inakisiwa alizaliwa mwaka wa 1119 kabla ya Yesu. Je, samsoni alifariki lini? Hatujui kwa uhakika, lakini inakisiwa alifariki mwaka wa 1079 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 5



### UKWELI AMA UONGO

Chora alama ya mduara kwenye umbo iwapo jibu ni sahihi na umbo iwapo jibu sio sahihi.

1. Nguvu ya Samsoni ilitoka kwenye moyo wake.
2. Delilah alimsaliti Samsoni na kumtoa kwa Wafilisti.
3. Wafilisti wengi walifariki wakati Hekalu lilibomoka naye Samsoni alibaki hai.
4. Samsoni alikuwa na nguvu hata bila nywele.
5. Samsoni aliua maelefu ya watu akitumia mfupa wa punda.

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| D | S | I | N | O | S | M | A | S | A | A | M | S |
| E | I | T | M | F | D | E | L | I | L | A | N | N |
| L | M | S | G | N | K | A | M | B | L | P | Y | G |
| U | F | I | Y | N | A | G | N | A | D | U | W | I |
| O | B | L | I | G | M | D | I | G | W | F | E | D |
| T | A | I | F | N | B | K | H | L | U | M | L | A |
| O | H | F | U | A | A | B | M | I | S | V | E | H |
| T | M | A | M | L | A | K | A | U | R | W | U | A |
| M | N | W | A | F | O | G | N | A | L | I | M | N |

## MASWALI NA MAJIBU YA 5

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, naweza kufanya mambo nipendavyo? (Kama tunataka kumheshimu Yesu, tunafaa tufanye mambo jinsi anavyotaka. Hata ingawa uokozi ni zawadi ya bila malipo, lakini tunasalimu nafsi yetu yote kwa Mungu, ikiwemo maelezo ya maisha.)
2. Watu wazuri wanaenda mbinguni, au sio? (Jadiliana kuhusu tofauti ya kuwa mzuri au kuruhusu uzuri wa Yesu Kristo kufidia dhambi zetu. Hakuna mtu mzuri vinavyofaa.)
3. Mbona nimwamini Mungu? (Mungu ndiye pekee tunayeweza kuamini. Mababa zetu, wahubiri, na walimu watatukosea mara kwa mara. Ni jambo chungu, lakini mwishowe, tunafaa kumwamini Mungu tu.)

## MCHEZO WA 5

**Kumakinika**



Watoto wataketi na kuunda mduara, na kisha mmoja atakwenda katikati na kujaribu kukisia kiongozi ni nani. Kiongozi atachaguliwa bila mtoto aliye katikati ya mduara kujua ni nani. Kiongozi aliyechaguliwa ataanza kurudia tendo fulani, na kisha watoto hao wengine watarudia tendo hili, bila ya yule aliye katikati kugundua ni nani aliyeanza. Vitendo hivyo vinafaa kuwa rahisi, kama vile, kumgusa mwingine kichwa, kumgusa pua, sikio, na kadhalika. Baada ya aliye kutambua kiongozi ni nani, watabadilishana nafasi na kisha watacheza tena.

## MAHUDHURIO YA 5




Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Samsoni**

## KAZI YA 5 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kazi yako ya ziada wiki hii itakuwa ni kuchunguza mambo kuhusu maisha. Je, unatii wazazi wako? Je, una uhusiano mwema na watu? Je, umesamehe kila mtu? Je, kuna kitu unachoficha walio juu yako ( wazazi, mwalimu, mhubiri, nk)? Chagua kielezo unachokosa, omba Mungu akusamehe na akusaidie, mweleze aliye juu yakona kisha ulitubu. Makinika katika kufanya kinachofaa kwa kutumia kielelezo hiki katika siku zinafouta wiki nzima.

**Soma**

Siku ya 1: Ruthu 1:1-7
Siku ya 2: Ruthu 1:11-18
Siku ya 3: Ruthu 2:1-4
Siku ya 4: Ruthu 2:19-23
Siku ya 5: Ruthu 4:9-15

# 6. MUNGU ANAKUBARIKI



**Haditi ya Biblia: Ruthu**
Ruthu 1:1-3:3, 3:16-4:22

## FUNGU LA 6 LA KUMBUKUMBU

"Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea BWANA, Ambaye BWANA ni tumaini lake." Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, Uenezao mizizi yake karibu na mto; Hautaona hofu wakati wa hari ujapo, Bali jani lake litakuwa bichi; Wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, Wala hautaacha kuzaa matunda. Yeremia 17:7-8

## HADITHI YA 6 YA UHITAJI



Leo shuleni, mwalimu wake Comet alipendekeza jambo kwa kikundi chote. "Ningependa kila siku baada ya masomo yetu mnisaidie kufanya usafi humu darasani na kupanga vifaa. Halafu tunaweza kumaliza kwa haraka na kuondoka kuelekea nyumbani. Iwapo kila mtu atanisaidia, wakati wa kufunga shule, ntampa tuzo." Kila mtu alipenda pendekezo hilo akiwemo Comet, lakini ilikuwa ngumu kiasi kwani yeye aliishi mbali ikilinganishwa na wengine. Hata hivyo, kila mtoto alianza kubaki. Halafu baada ya muda, wakafikiria sio vyema kubakia, kwani zawadi huenda ingekuwa ni ndogo mno. Lakini Comet hakukoma kumsaidia mwalimu katika lolote. Alikuwa hapo kila wakati, bila kuwaza sana kuhusu zawadi.

## SOMO KUU LA 6

Karibu tena! Wakati wa waamuzi kama vile, Jephta na Samsoni, kulikuwa na hadithi nyingine nzuri. Mwanaisraeli mmoja alihamia na familia yake hadi Moabu kwa sababu ya ukame. Baada ya muda wa miaka 10, wote baba na watoto walifariki. Tunaishi katika ulimwengu uliojaa dhambi, na vitu vibaya vimekuwa vikwawatendekea Wakristo na pia wale ambao sio Wakristo. Yesu alisema kuwa tungepitia shida lakini akahakikisha angekuwa nasi wakati wote. Mjane Naomi alirudi Israeli na wakwe wake wawili, Ruthu na Orpa. Wakiwa safarini, Naomi aliwataka warudi Moabu, akifikiria kungekuwa kuzuri. Walipendana sana na shughuli ya kuachana ilikuwa yenye hofu nyingi. Orpa alirudi Moabu, lakini Ruthu hakumwacha Naomi, na kusema kwamba watu na Mungu wa Naomi, wangekuwa ndio watu na Mungu wake pia. Naomi alisema maisha yake kule nyumbani Bethlehemu yalijawa na shida na uchungu. Tunapopitia jambo gumu au matataizo, ni rahisi kujawa na uchungu moyoni. Lakini Ruthu alibaki na Naomi, na kufanya kazi naye kwa bidii katika shamba la Boazi kukusanya shayiri. Halafu mamake-mkwe alipomwamurisha kufanya lolote, alitii bila pingamizi yoyote. Uaminifu, bidii na utiifu, ni vitu vizuri sana mbele ya Mungu hata kuliko nguo nzuri, nywele au mapambo na vifaa. Boazi pia aligundua hili. Alimwambia Ruthu aendelee kufanya kazi katika shamba lake na kwamba angemlinda. Alikuwa mwenye roho nzuri na mkarimu, na alimwalika kula naye vyakula vya mchana na kumpa vyakula vingi. Ulipofika wakati wa kuoa, Boazi alisimamia kila kitu na kwa njia iliyompendeza Mungu. Wema, ukarimu na uadilifu vyote vinaonyesha Yesu, bali sio nguvu na utanashati. Biblia inasema tukimuenzi Mungu na kumtambua kama mwenye umuhimu na mwenye maana maishani mwetu, anatupa tunachokitamani. (Zaburi 37:4) Yesu alisema kwamba yuaja kutupa maisha maneefu. (Yakobo 10:10) Yesu pia alisema tunapompa kila kitu, anatuzawadi mara mia moja, zingine katika maisha haya na zinginezo mbinguni! (Mathayo 19:28-30) Mungu anataka kutubariki. Boazi na Ruthu walioana na wakabarikiwa na mvulana mchanga aliyeleta

furaha kubwa kwa Naomi. Mara nyingine, Baraka zetu kutoka kwa Mungu, zinasaidia watu wengine pia. Baozi na Ruthu wakawa ni mababu wa mfalme Daudi na wazazi wa kale wa Yesu. Baraka ya Mungu inaweza kuja maishani mwako kwa njia ya familia, au rafiki unayetaka kuwa naye, ama kazi nzuri, au nafasi kubwa za kumtumikia Mungu. Baadaye leo, tutaona kwamba Comet pia alibarikiwa. Mungu pia anatumia vitu tofauti vidogo ili kukudhihirishia kwamba anakupenda. Mungu anataka kukubariki, na unapo mweka Mungu mbele na kumuenzi, na kuishi jinsi anavyotaka hata wakati mgumu, Mungu atakubariki.

Naamini Mungu anataka kunibariki, na nitafanya kila niwezalo ili kumfuata bila kujali lolote.

## SULUHISHO LA 6

Siku ilifika, na mwalimu alimpa Comet zawadi, kwa sababu alikuwepo kila wakati kumsaidia. Je, unafikiria alimpa nini?




Lo! Baiskeli! Ilikuwa ni zawadi nzuri sana kwa Comet, kwa sababu kwa kuitumia aliweza kufika nyumbani haraka na bila kuchoka sana.

## SHUGHULI YA 6

**Kikumbusho**

Kazi ifuatayo ni ya wanafunzi kukumbuka kitu ambacho Mungu amewabariki nacho.

Chukua karatasi aina ya A4 na uikunje, kama ilivyoonyeshwa kwenye mchoro. Weka nafasi ambapo watachora au kuweka picha. Kama una picha nyumbani, unaweza kukata nafasi ya kuitia. Picha zenyewe zinaweza kuwa ni za watu wa familia yako au kitu unachokimiliki na unakienzi sana.





## MSTARI WA 6 WA WAKATI

Je, hadithi ya Ruthu ilifanyika lini? A. Hatujui wakati halisi, lakini inakisiwa kwamba ilikuwa mwaka wa 1230 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 6





| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | A | C | H | U | N | G | U | M |
| I | M | O | A | B | U | F | S | U |
| Z | A | I | D | I | I | N | H | H |
| A | L | V | R | N | J | T | A | C |
| O | U | Z | I | A | U | I | Y | B |
| B | K | M | A | R | K | R | I | O |
| B | A | R | A | K | A | U | R | R |
| U | Y | U | K | A | R | Z | I | P |
| N | V | Y | S | H | A | M | B | A |


## MASWALI NA MAJIBU YA 6

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, mimi nafaidika na nini? (Mungu ni mkarimu, na anapenda kutubariki. Ndoto zako kubwa ni gani? Subiri miaka kadhaa ushuhudie Mungu akizitimiza! Chunguza kwa makini kile wanafunzi wako wanatamani, gari jipya, ama simu mpya, nk. na uwasaidie kuwa na ndoto za vitu bora na vyenye umuhimu.
2. Kama Mungu anataka kutubariki, mbona anakubali maovu yatendeke? (Tunaishi katika ulimwengu uliojaa dhambi, na maovu huwa yanatendekea kila mtu. Pia, Mungu anajali roho zetu kuliko miili yetu. Roho na mioyo yetu ni za milele, lakini mwili utaisha. Mungu anatumia hali chungu na ngumu ili kubadilsha roho zetu na kuzifanya kukomaa.
3. Mbona kila mtu anasema "Mungu akubariki" kanisani? (Huenda ikawa ni kawaida, salamu rahisi, lakini kwa sababu kila mtu amezoea … mbona hata wewe usichangie?)

## MCHEZO WA 6

**Baraka mbalimbali**




Mtu mmoja ni muuzaji, na mwingine ni mnunuzi na vingine ni Baraka. Mwalimu atawapa watoto majina ya Baraka (mifano ipo hapo chini) Mnunuzi atakapowasili, atasema; nataka zawadi. Naye mwuuzaji atasema Je, unatafuta Baraka gani? Unaweza kuchagua kutoka kwa orodha hii. Mnunuzi atauliza, Je, inauzwa pesa ngapi? Kama hio Baraka ipo, mtoto aliyepewa jina la hio Baraka atasema umri wake kwa sauti kubwa, na kisha atakimbia ili asishikwe. Mnunuzi atalipa kwa kupiga makofi kuwakilisha umri wa mtoto huyo na kisha wote wawili watamkimbiza na kujaribu kumshika. Iwapo atashikwa, mtoto aliyeshikwa atapoteza, na iwapo hatashikwa, basi atarudi na kupewa jina lingine. Baraka zinaweza kuwa ni:

1. Vyakula
2. Uokovu
3. Afya
4. Baga
5. Nguo
6. Peremende
7. Keki
8. toy
9. Amani
10. Maarifa
11. Furaha
12. familia
13. upendo
14. Marafiki
15. Uhai wa milele

Ukipenda: Unaweza kuchagua meza, kiti, mti, au jiwe kuwakilisha ghala ndogo.

## MAHUDHURIO YA 6




Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Ruthu**

## KAZI YA 6 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kazi yako ya ziada wiki hii ni kuwaza kuhusu kitu unachokimiliki na unakipenda, Kwa mfano, familia yako, rafiki, nyumba au kitanda chako, kipenzi, somo unalopenda shuleni, nk. Shukuru Mungu kwa kitu hiki kila siku ya wiki hii.

**Soma**

Siku ya 1: 1 Samweli 1:1-8
Siku ya 2: 1 Samweli 1:9-20
Siku ya 3: 1 Samweli 3:1-6
Siku ya 4: 1 Samweli 3:7-14
Siku ya 5: 1 Samweli 3:15-21

# 7.MUNGU ANAKUCHAGUA



**Hadithi ya Biblia: Samweli**
1 Samweli 1:1-28, 3:1-21

## FUNGU LA 7 LA KUMBUKUMBU

“Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu  awapeni.” Yohana 15:16

## HADITHI YA 7 YA UHITAJI



Katika Kanisa la Comet, wanakwenda katika Shule ya Likizo ya Biblia. Watoto wote walipangwa kufanya michezo ya kuigiza, na vitu vingine. Wote walielekezwa na mwalimu wao wa kanisani, lakini Comet, hakuwa na jambo la kufanya. Aliingiwa na hofu nyingi na kudhani hakuwa na dhamana yoyote, kwamba Mungu hawezi kumtumia au hatamtumia.

## SOMO KUU LA 7

Karibu tena kwa Mashujaa wa Imani! Leo, tutasoma kuhusu Samueli, ambaye alikuwa muamuzi wa mwisho wa Israeli, na jinsi Mungu alivyomuita. Unakumbuka wanaume na wanawake wa imani ambao tumesoma kuwahusu? Je, unafikiria Samueli alikuwa ni mtu wa aina gani: Shujaa mashuhuri, tajiri, au kuhani? Wacha tutambue jinsi ambavyo Mungu alimwita. Mwanamke mmoja huko Israeli hangeweza kupata watoto, na ilimtia hofu kubwa. Siku moja alipokwenda na mumewe katika hekalu, aliomba kwa moyo Mungu aweze kumbariki na mtoto, na kusema angempa Mungu mtoto Yule. Baada ya kwenda nyumbani, Mungu alijibu maombi yake, na akapata mvulana mchanga aliyeitwa Samueli. Alimpeleka Samueli kwenye hekalu na kumweka chini ya ulezi ya kuhani aliyeitwa Eli, Samueli alilelewa hekaluni. Siku moja Samueli alipokuwa mchanga, alikuwa amelala kwenye hekalu, alikuwa akichunga mishumaa. Wakati wa usiku, aliskia mtu akimwita Samueli! Samueli! Aliamka na kukimbia alikuweko Eli na kumwambia Nipo Hapa! Lakini Eli hakuwa amemwita. Baada ya kuitwa mara tatu, Eli aligundua kwamba ilikuwa ni Mungu aliyekuwa akimwita. Alimwambia Samueli arudi na amsikize Mungu. Mara nyingine Mungu alipomwita Samueli alisema “Nipo hapa” Mungu anapotaka kufanya mambo mazuri katika ufalme wake, mara nyingine tunafikiri kwamba Mungu atatumia malaika ambao watashuka na kutuongelesha kwa sauti kubwa. Mungu amefanya haya mawili, lakini Mungu anawatumia watu wa kawaida kama mimi na wewe! Mungu hataki kuwatumia wahubiri pekee, au wachungaji, au walimu. Mungu anataka kukutumia pia kama mtoto mahali ulipo! Baadaye tutaona jinsi Mungu alimchagua Comet kwa ajili ya hadithi ya mapema hii leo. Yesu, alisema kwamba kondoo wake, (wewe) anaweza kuskia na kuitambua sauti yake. (Yohana 10: 27) Ili kuwa tayari kuitwa na Mungu kama Samueli, tumia wakati wako kanisani na usaidie popote unapoweza. Waombe maarifa walimu, wazazi na wahubiri wako, ambayo yatakusaidia kuitambua sauti ya Mungu. Halafu Mungu atakapokuita umjibu “Nipo Hapa” Na ufanye kile atakachokwambia. Baada ya Samueli kupata ujumbe kutoka kwa Mungu, alilala usiku wote na kumwambia Eli ilipofika asubuhi. Iwapo Mungu atakuita ukikula kwenye hoteli, usiingilie kile kila mtu anachofanya ili uweze kuingia kwenye hali ya roho. Kwenda

kwenye choo na uombe. Inakaa ni upumbavu, lakini Mungu anaweza kukuongelesha mahali popote. Halafu unaweza kurudi na kuwaambia wazazi au mwalimu wako kuhusu jambo hili katika wakati mwafaka. Samueli alifunza kuhusu neno la Mungu kwa imani katika maisha yake yote. Alikuwa mwamuzi wa mwisho wa Israeli, na Mungu alimtumia kuwachagua Wafalme wawili wa kwanza wa Israeli.

Nachagua kuwa tayari, Mungu atakaponiita.

## SULUHISHO LA 7


Alikwenda kusikiliza katika Shule ya Likizo ya Biblia. Lakini siku moja alimpata mvulana mdogo katika masomo yale akilia, mvulana yule alisema kwamba hakuna mtu aliyemtaka. Comet alimwambia kuhusu neno la Mungu, na kwamba Mungu alimpenda na kwamba Mungu alikuwa naye kila wakati. Comet alimwalika kanisani, na kutoka ile siku, mvulana huyo na mamake hawajakosa kwenda kanisani. Ni hapo ambapo Comet alitambua kwamba Mungu alimtaka kuwa mmoja wa wanajeshi wake.



## SHUGHULI YA 7

**Kuitwa**

Andika kwenye karatasi jinsi unavyodhani Mungu anaweza kukuita katika umri wako au katika hali yako. Mifano: Kukuita kupitia Biblia, mwalimu, kusaidia katika tukio fulani kanisani, kumsaidia mwanafunzi mwenzako ambaye utamwona akilia, na anayesema anajihisi bila dhamana au anayechukia maisha yake.




## MSTARI WA 7 WA WAKATI

Je, Samueli alianza kuongoza Israeli lini? A. Hatuna mwaka halisi, lakini inakisiwa alianza kuongoza mwaka wa 1143 kabla ya Yesu.

Je, samueli alifariki mwaka mgani? A. Hatuna mwaka halisi, lakini inakisiwa kwamba alifariki mwaka wa 1055 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 7





| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | U | F | I | N | I | M | A | A | T |
| U | L | A | L | A | O | I | T | I | I |
| I | J | U | E | L | I | T | W | K | I |
| I | T | U | W | A | U | K | I | S | U |
| I | Z | U | M | A | W | M | R | W | J |
| S | N | G | A | B | Z | A | Z | P | U |
| R | A | N | S | S | E | I | K | Y | M |
| A | B | U | T | L | A | L | K | C | D |
| E | L | M | I | I | B | A | N | S | E |

## MASWALI NA MAJIBU YA 7


**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Lakini naweza kuleta mabadiliko gani? (Ni jambo la kustajaabisha kuona mambo ambayo mtu anaweza kufikia. Hata ingawaje tunakaa wadogo, tunaweza fanya makuu. Itasaidia ukichukua muda na kusahau tarakimu kubwa, mamilioni ya watu walio na njaa, na uzingatie mtu mmoja. Je, kuna mtu karibu nawe ambaye anahitaji usaidizi? Kumsaidia mtu MMOJA kutatusaidia kuanza… kasha mtu mwingine… na mwingine… na baada ya muda muda mfupi utakuwa sehemu ya mabadiliko MAKUBWA!
2. Mbona hakuna vyakula na pesa za kutosha kwa kila mtu ulimwenguni? (Wasaidie wanafunzi wako kuwaza kuhusu hali hii. Labda Mungu anataka tujifunze jinsi ya kushiriki na wengine? Labda ni sehemu ya dhambi iliyoingia ulimwenguni kupitia Adamu.)

3. Je, itakuwaje kama mtu fulani ananichukia? (Hatuwezi kuwa na urafiki na kila mtu, lakini Mungu anataka tuwasaidie hata adui zetu. Nani ajuaye? Labda Mungu na mipango mikuu juu ya kila mtu, na anapanga kukutumia!)

## MCHEZO WA 7

**Bweha na Kondoo**



Wanafunzi wataunda mduara huku wakishikana mikono. Mpe mtoto mmoja jukumu la kuwa mbweha na mwingine kondoo. Kondoo atakuwa ndani ya mduara na mbweha atakuwa nje, wanafunzi waliotengeneza mduara hawatamkubalisha mbweha kumkamata kondoo. Mbweha atajaribu kumshika kondoo kwa kujaribu kuingia kwenye mduara, iwe ni kupitia juu au chini au kwa kuvunja mduara. Iwapo mahali kuna jozi la watoto wawili watamruhusu mbweha kuingia basi watatolewa kwenye mduara. Kondoo na mbweha wanaweza kuingia na kutoka kwenye mduara.




## MAHUDHURIO YA 7

Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Samweli**

## KAZI YA 7 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kazi ya ziada wiki hii ni kufanya kitu chenye huruma kila siku, kwa mfano kumsaidia mtu mzee kuvuka barabara, kumsaidia mtu mzima vitu vyake kutoka kwa duka, kumsaidia mwanafunzi mwingine na kazi yake ya ziada shuleni, etc.Wakati wa darasa lingine, Mwambie mwalimu wako kuhusu vitendo hivi.

**Soma**

Siku ya 1: 1 Samweli 5:1-6
Siku ya 2: 1 Samweli 5:7-12
Siku ya 3: 1 Samweli 6:1-6
Siku ya 4: 1 Samweli 6:7-12
Siku ya 5: 1 Samweli 6:13-16, 7:1

# 8. MUNGU NI MWENYE NGUVU ZOTE



**Hadithi ya Biblia: Sanduku la Agano.**
**1 Samweli 4:1-11, 5:1-6:21**

## FUNGU LA 8 LA KUMBUKUMBU

"Kwa maana BWANA, Mungu wenu, yeye ndiye Mungu wa miungu, na Bwana wa mabwana, Mungu mkuu, mwenye kuogofya, asiyependelea nyuso za watu, wala hakubali rushwa." Kumbukumbu la Torati 10:17

## HADITHI YA 8 YA UHITAJI



Kip alikuwa kanisani na rafikiye siku moja, na rafikiye alilia kwa sababu aliumwa na kichwa. Halafu Kip alifikiria kumwombea, ili kuona kama angepona. Aliomba kwa wakati mfupi, na je unadhani nini kilifanyika?...

Rafikiye hakuhisi maumivu tena! Kutoka ile siku, Kip alidhani alikuwa na nguvu za kuponya wagonjwa, na akasahau kwamba haikuwa uwezo wake, bali ulikuwa ni uwezo wa Mungu. Aliwaringia wanafunzi wenzake shuleni kuhusu uwezo wake.

## SOMO KUU LA 8

Wiki iliyopita, tulisoma kwamba Mungu anapenda kuwatumia watu kufanya mambo mazuri. Wiki hii tutasoma kwamba, Mungu, hawahitaji watu. Katika siku za zamani, Uwepo wa Mungu ulikuwa na Wanaisraeli kwenye Sanduku la Agano. Ndani ya Sanduku hili, kulikuwa na mawe mawili ambayo yaliandikwa Amri kumi, kijiti cha Aaroni, na kifaa kilichotiwa mana au mkate kutoka mbinguni ambayo Wanaisraeli walikula wakiwa kwenye jangwa. Baada ya Mungu kumwita Samueli, ambaye tulisoma kumhusu wiki iliyopita, wanaisraeli walikuwa katika vita vikubwa na Wafilisti. Wanaisreali walishindwa katika vita vya kwanza, halafu wakaleta sanduku la agano, kwani walidhani kwamba wangeshinda kwa sababu Mungu angekuwa nao. Mara nyingine, tunafikiria Mungu anafaa kufanya kila kitu jinsi sisi tunavyomtaka, kama alivyofikiria Kip, katika hadithi ya leo. Lakini Mungu hayupo kwenye chupa akingoja maelekezo. Mungu ni mwenye nguvu zote, yupo kila mahali na anajua kila kitu, na atahakikisha anachotaka kimetendeka. Siku ya pili ya vita, jeshi la Wanaisraeli lilishindwa, na Wafilisti waliteka Sanduku la Agano. Wanaisraeli waliingiwa na hofu nyingi. Mara nyingine, tunajali kuhusu sifa za Mungu, lakini Mungu ni mkuu na anaweza kujitetea. Wafilisti walichukua Sanduku hilo na kuliweka katika hekalu chini ya sanamu yao ya joka. Asubuhi, sanamu ile ya joka ilikuwa imeanguka kichwa kwanza, mbele ya Sanduku lile la agano! Waliisimamisha tena, lakini asubuhi iliyofuata ilikuwa imeanguka tena na mikono yake ilikuwa imevunjika. Zaidi ya hayo, ugonjwa wa kufura ulianza katika mji huo. Mungu ni mwenye nguvu zote na ana uwezo wa kupigana vita vyake. Wafilisti walipeleka Sanduku hilo katika miji mitatu tofauti na kila katika mji, kulizuka ugonjwa wa kufura. Halafu walilitia Sanduku lile kwenye mkokoteni, pamoja na dhahabu kiasi, na ng'ombe waliukokota hadi Israeli. Mungu aliwaongoza ng'ombe wale bila usaidizi wa mtu yeyote. Sanduku lilipofika Israeli, watu walishangilia lakini wengine walifariki kwa kutizama ndani yake. Yesu alisema kwamba tunafaa kumwogopa Mungu pekee - lakini Mungu pia ni baba yetu anayetujua kwa undani hadi nywele zilizopo kichwani mwetu. Anatupenda na atatulinda. Hatufai kujali kuhusu lolote. Katika siku za zamani, uwepo wa Mungu ulikuwa katika Sanduku. Lakini sasa

kwa sababu ya Yesu, uwepo wa Mungu umejaa katika roho zetu. (1 wakorintho 16:9 ) Yesu alitimiza yale yalimokuwa kwenye sanduku, Yesu alitimiza amri kama mawe yaliyokuwemo, yeye ni kiongozi wetu kama vile kijiti cha Aaroni kilivyowakilisha, na ni mkate wetu wa kila siku kama mana kutoka mbinguni. Nyoosha kidole kwenye roho yako. Ukimwamini Yesu, unakuwa kama Sanduku la Mungu la agano! Mungu wetu mwenye nguvu yote anaingia ndani yako na kuishi ndani yako na anakwenda nawe popote unapokwenda.

Naamini kwamba Mungu ni mwenye nguvu, na nitamheshimu. Nachagua kumfanya Yesu mfalme wangu na kutojali kitu chochote.

## SULUHISHO LA 8



Siku moja mwanafunzi mwenzake shuleni alikuwa akiumwa na sikio. Kip alimwambia kwamba angemwombea, na kwamba uchungu ungeisha mara moja. Kip alimwombea, lakini hakuna kilichofanyika. Kip alihisi kuaibika; alizungumza na mwalimu wake wa kanisani kuhusu kilichofanyika. Mwalimu wake alimwelezea kwamba nguvu inatoka kwa Mungu pekee.

## SHUGHULI YA 8

**Mafungu ya maneno**

Mpe kila mtoto karatasi yenye nafasi tano, kama iliyoonyeshwa hapo chini. Zikate na kisha uandike maandiko ya Biblia yanayozungumzia kuhusu nguvu na uwepo wa Mungu, kama vile Zaburi 23:1 Marko 10:27 na kadhalika.

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |


## MSTARI WA 8 WA WAKATI

Je, ni mwaka upi ambapo wafilisti waliliteka Sanduku la Agano? A. Hatujui mwaka halisi, lakini inakisiwa ilikuwa ni mwaka wa 1142 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 8



| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | W | E | N | Y | E | N | G | U | V | U | Z | O | T | E |
| K | M | E | B | N | I | V | T | E | A | G | O | N | A | I |
| O | K | U | T | O | T | I | I | M | B | T | B | I | I | S |
| K | B | K | W | M | W | M | R | F | I | M | M | B | O | A |
| O | E | U | A | U | T | I | T | S | I | L | I | F | A | W |
| T | R | D | F | N | G | O | M | B | E | S | F | V | I | I |
| E | O | N | A | G | A | A | L | U | K | U | D | N | A | S |
| N | H | A | M | U | N | M | G | U | B | I | B | L | I | A |
| I | O | S | R | V | I | M | E | T | O | K | O | K | M | W |



## MASWALI NA MAJIBU YA 8

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, Mungu huyu aliye na nguvu na ukuu anaweza aje kuwa rafiki yangu? (Mungu anahusu mengi. Tunapaswa kumwogopa, ila ni vizuri pia kujua kwamba anatupenda. Biblia inatwambia kwamba Mungu anajua idadi ya nywele vichwani mwetu, anajua hadi maelezo yale madogo zaidi.)
2. Mbona nahisi Mungu yupo mbali nami? (Kuanzia mwanzo, IMANI imekuwa kitu muhimu sana kwa Mungu. Mungu anataka tumuamini hata ingawa hatumuoni. Labda ilikuwa ni mpango wake kutuumba sio kama roboti ili tutende mazuri tu. Kama tunaweza kuwona Mungu jinsi alivyo, sisi sote tungempigia magoti. Wakati mwingine inaonekana kana kwamba hatuwezi kumwona Mungu na yuko mbali nasi, lakini Mungu anaziona roho zetu na anajua ni nani mwenye imani.)
3. Je, kweli kutakuwa na mwisho wa ulimwengu? (Zungumza na wanafunzi wako kuhusu mada hii, hitimisha kwaba ni KWELI. Tukiamini Biblia kwa ukweli, lazima tutambue kwamba kutakuwa na mwisho wa ulimwengu tunavyoujua.)


## MCHEZO WA 8

**Kiazi Moto**



Wanafunzi wote waunde mduara. Muziki unapocheza, wanafunzi wanafaa kupitisha kifaa kuzunguka mdaura huu. Muziki utakaposimamishwa, mtoto atakayekuwa na kifaa mkononi mwake atatoa ushuhuda kuhusu alichokitenda Mungu maishani mwake. (Kwa mfano, Mungu alipomlinda kutokana na mtoto aliyemsumbua, au wakati Mungu alimpa vyakula, pesa, na kadhalika.)

## MAHUDHURIO YA 8




Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Sanduku la Agano**

## KAZI YA 8 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kazi yako ya zaida wiki hii ni kutafuta kiberiti kitupu au chombo kingine kidogo. Unaweza kukipamba. Andika fungu za Biblia kwenye vipande vya karatasi, weka vipande hivi ndani ya chombo hiki na ukitie mfukoni. Kila wakati unapata shida, unarejelea vile vifungu. Halafu neno la Mungu litakufariji maishani mwako. Beba chombo hiki wakati wa somo lingine na ukionyeshe kwa mwalimu.

**Soma**

Siku 1: 1 Samweli 8:4-11, 17-22
Siku 2: 1 Samweli 9:1-9
Siku 3: 1 Samweli 9:25-10:2
Siku 4: 1 Samweli 10:9-11, 17-25
Siku 5: 1 Samweli 13:1-14

# 9.MAPENZI YA MUNGU



**Hadithi ya Biblia: Mfalme Sauli**
1 Samweli 8:4-21, 9:15-10:1, 10:20-25, 13:5-14, 15:1-31

## FUNGU LA 9 LA KUMBUKUMBU

"Unifundishe kuyatenda mapenzi yako, Kwa maana ndiwe Mungu wangu; Roho yako mwema aniongoze kwenye nchi sawa." Zaburi 143:10

## HADITHI YA 9 YA UHITAJI



Kip anaskia hofu kwamba babake hamruhusu kwenda nje na anamwadhibu kila anapokwenda kucheza na watoto wengine mahali anapoishi. Kip anajua kwamba watoto hawa hawana tabia nzuri. Kisha siku moja, Kip alizungumza na mhubiri wake, na kusema kwamba hataki tena kumtii baba yake, kwa sababu babake sio mtu mzuri. Halafu mhubiri akamwuliza, "Mbona unasema hivyo?" Kip akamjibu," Kwa sababu haniruhusu kwenda nje kucheza na ananiadhibu kila mara."

## SOMO KUU LA 9

Wiki iliyopita, tulisoma kwamba Mungu ni mwenye nguvu zote, na kwamba anapanga kufanya kile anachotaka. Leo, tutasoma kuhusu mtu aliyeitwa Sauli, na kile hutendeka tunapojaribu kubadilisha azimio la Mungu, ua tunapokosa kutii akitakacho Mungu. Katika siku hizo, Israeli haikuwa na Mfalme na Samueli alikuwa bado ndiye kiongozi wa Israeli. Wanaisraeli, walikwenda kwa Samueli na kumtaka kumchagua mfalme kama nchi zao jirani. Ni rahisi kuangalia wanachomiliki majirani wetu. Tunapoanza kulinganisha, tunakosa kutosheka na kile Mungu alitochotupa. Wanaisraeli walimwomba Mungu kuwapa Mfalme. Lakini Mungu aliwaonya kwamba halingekuwa jambo nzuri kwao, na lingekuwa ni jambo ambalo hawangeweza kulibadilisha.

Mungu anatupenda na anatutakia mazuri, lakini mara nyingine tunajaribiwa kumwomba Mungu vitu vingine, Mungu alikubali na akamtuma Samueli kumchagua mtu aliyeitwa Sauli kama mfalme. Lakini wakati ulivyoendelea, Sauli alianza kukosa kumtii Mungu. Kama hadithi ya hapo awali, kutotii kunaweza kutuingia, na tunafaa kumakinika! Yesu alisema tukae macho na tuombe ili tusiingie katika majaribu. (Mathayo 26: 14) katika vita fulani, Sauli alifaa kumngoja Samueli ili atoe dhabihu kwa Mungu, jambo ambalo ni walevaiti kama Samueli pekee walipaswa kufanya. Walingoja karibia wiki mzima na wakachoka kungoja. Sauli aliogopa kwamba angepoteza jeshi lake, alidhani kwamba watu walikuwa na umuhimu kuliko Mungu katika kushinda vita. Alikosa kutii amri ana akatoa dhabihu yeye mwenyewe. Samueli alimwambia kwamba Mungu tayari alikuwa akimtafuta mtu mwingine mzuri, ili kuchukua nafasi yake ya ufalme. Unapokoma kumtii Mungu, unaweza kuwa ukiachilia kitu muhimu ambacho Mungu angekupa. Kwa sababu ya kifo cha Yesu msalabani, tunayo neema ya Mungu ya kutuongoza kila wakati. Badala ya kukosa kutii, muombe Mungu akusaidie. Baadaye, Sauli alikosa kutii amri ya Mungu ya kuwavamia Wamalekaiti, na alimnusuru mfalme na kondoo na ng'ombe wale wazuri. Alisema kuwa angewatoa wanyama hao kama dhabihu kwa Mungu, lakini Samueli alisema utiifu ni bora zaidi kuliko dhabihu. Katika maisha yetu pia, na hata ingawaje ni vyema kumpa Mungu wakati wetu, pesa, zawadi, na kadhalika, Mungu kila wakati anachagua utiifu. Yesu alisema kwamba yeyote anayemtii Mungu ni

kakake au dadake. (Mathayo 12:50) Yesu pia alisema kuwa Mungu anajali zaidi kufanya azimio lake kuliko unabii, kutoa mapepo, au kufanya miujiza. (Mathayo 7: 21- 23) Kwa sababu ya Sauli kukosa kutii, Mungu angemnyang'anya ufalme na katika maisha ya Sauli, alikosa kutii hata zaidi, na aliuawa katika vita. Wakati mwingine tutasoma kuhusu mtu mwingine aliyechukua nafasi ya Sauli kama mfalme, mtu aliyemakinika zaidi kufanya jambo lililofaa kila wakati.

Nachagua kumtii Mungu na kufanya anachotaka, chochote anachotaka nifanye.

## SULUHISHO LA 9



Mhubiri alizungumza na Kip, na kumweleza kwamba babake, anamtakia mazuri na kwamba anapaswa kumtii babake kwa sababu ndiye mwenye mamlaka mle nyumbani. Hapo ndipo Kip alianza kufikiria alichoambiwa na mhubiri, na akagundua mhubiri alisema kweli, na kwamba babake alikuwa akimlinda kutokana na watu ambao wanangemfanya kuwa mtovu wa maadili.

## SHUGHULI YA 9

**Kioo**

Shughuli hii itafanya watoto wazungumze baina yao na kuwasaidia kujuana. Maagizo:

1. Mtu anayesimamia shughuli hii anafaa kuwaweka watu wawili pamoja.
2. Watoto wawili waliowekwa pamoja wanafaa kusimama mbele ya yule mwingine.
3. Kuanzia, mtoto wa kwanza atajaribu kuiga matendo ya yule mwingine kama kioo, bila kujali sehemu ya mwili wanayoitumia (anaweza kuiga vitendo, kusogeza mikono, miguu na kadhalika.)
4. Kisha utakuwa wakati wa yule mwingine wa kumuiga.



## MSTARI WA 9 WA WAKATI


Je, Sauli alizaliwa mwaka gani? A. Hatujui kwa uhakika, lakini inakisiwa ilikuwa mwaka wa 1082 kabla ya Yesu.

Je, sauli alifariki mwaka gani? A. Hatujui kwa uhakika, lakini inakisiwa ilifariki mwaka wa 1010 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 9



| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| T | M | F | A | L | M | I | B | M | B | U | A |
| O | U | S | U | T | I | I | F | U | D | D | W |
| O | T | G | A | T | S | A | M | S | H | H | E |
| D | U | U | O | L | L | S | G | A | A | A | L |
| N | B | T | O | M | A | U | M | M | B | B | O |
| O | U | I | E | U | W | B | S | W | I | I | K |
| K | A | I | L | B | I | B | A | E | H | H | O |
| Y | E | I | N | G | O | J | A | L | Y | U | U |
| A | H | S | I | N | A | G | N | I | L | U | K |




## MASWALI NA MAJIBU YA 9

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, itakuwaje Mungu akitaka nifanye jambo lisilowezekana? (Mara nyingi, Mungu anataka kufanya muujiza maishani mwetu. Tunapaswa kuendelea kutii kile Mungu anataka tufanye, hatua kwa hatua.)
2. Je, Mungu alitoka wapi? (Biblia inasema kwamba Mungu amekuwepo wakati wote. Alikuwepo kabla ya kuwepo kwa ulimwengu, kabla sisi tuwepo na kabla ya kila kitu tunachojua. Mungu yupo, amekuwepo, na ataendelea kuwepo. Mungu ni wa milele.)
3. Je, mbona sio kila mtu anamwamini Mungu? (Shetani anatuongoza kwa njia isiofaa, anatuvuta mbali na Mungu. Zungumza na wanafunzi wako kuhusu jinsi watu tofauti wanasema kuwa wanamwamini Mungu, lakini maisha yao yanaonyesha kwamba hawamwamini. Je, matendo yetu yanadhihirisha nini kuhusu tunachokiamini?)


## MCHEZO WA 9

**Mpira wa Kuepuka**



Unda mraba mmoja sakafuni ukitumia kamba, riboni au mstari wa viti ulio na nafasi ya kutoshea timu mbili za watoto. Mtu mmoja atachaguliwa kuurusha mpira, na atawekwa katika sehemu tofauti katika mraba. Ili kucheza, warushaji wataurusha mpira kwa timu nyingine, na kujaribu kuwagonga, huku watoto walio katika mraba wakijaribu kuepuka kugongwa. Mtoto atakayegongwa na mpira ama kutoka kwenye mraba atatolewa kwenye mraba. Timu itakoyokuwa na watoto wengi ndani ya mraba ndiyo itakayoshinda.

## MAHUDHURIO YA 9




Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Manabii Wakku**

## KAZI YA 9 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kazi yako ya ziada wiki hii, kila wakati unapohisi kujaribiwa, omba Mungu akusaidie kufanya jambo linalofaa. Unapotenda dhambi, omba Mungu akusamehe na utubu. Pia, mwombe Mungu akusaidie kufanya vitu vizuri wiki hii, na kila wakati unapowaza kutenda jambo nzuri, kwa mfano kusaidia au kumpa mtu moyo, lifanye.

**Soma**

Siku ya 1: 2 Samweli 11:1-13
Siku ya 2: 2 Samweli 11:14-27
Siku ya 3: 2 Samweli 12:1-10
Siku ya 4: 2 Samweli 12:11-19
Siku ya 5: 2 Samweli 12:20-25

# 10.MUNGU HUTUADHIBU



**Hadithi: Mfalme Daudi**
**1 Samweli 16:1-13, 2 Samweli 5:1-5, 11:1-15, 12:1-23**

## FUNGU LA 10 LA KUMBUKUMBU

"Tazama, yu heri mtu yule Mungu amwadhibuye; Kwa hiyo usidharau kurudiwa na huyo Mwenyezi." Ayubu 5:17

## HADITHI YA 10 YA UHITAJI



Peppy anajua kwamba kuchukua kitu cha mtu mwingine ni makosa na kwamba jambo hili halimridhishi Mungu. Katika shule ya watoto ya Kanisa, kuna msichana fulani anaye tabia ya kuacha pesa sakafuni au juu ya meza. Kwa muda wa wiki tatu, Peppy alijizuia kuchukua pesa zile. Alifikiria, "Hakuna atakayejua nikichukua pesa hizi, - La! Sifai kufanya hivyo." Halafu siku moja aliwezwa na majaribu na alizichukua hela zile! Katika somo lingine, Peppy alimwona mvulana fulani akichukua kalamu ya mtoto mwingine. Alikasirika na akasema kwa sauti kubwa "Wewe! Umechukua kalamu za mwingine, kwani haujui ni makosa?" Na hata ingawaje mvulana yule aliomba msamaha na kurudisha kalamu zile, Peppy alishinda kuliongelelea jambo hili, na kuwaambia walimu na wasichana wengine karibu naye, na kumfanya mvulana yule kusikia vibaya sana.

## SOMO KUU LA 10

Wiki iliyopita tulisoma jinsi mfalme Sauli alivyokosa kumtii Mungu na akaendelea kumuasi. Leo, tutasoma kuhusu mtu aliyekuwa na kitu maalum. Mungu alimtuma Samueli hadi Bethlehemu ili kumchagua mfalme mwingine. Samueli aliridhishwa na nduguye mkubwa. Lakini Mungu alimweleza asiangalie sura kwa sababu Mungu huangalia roho. Mungu alichagua ndugu mdogo, Daudi, kama mfalme. Kama unajihisi mdogo au usiyetambulika, usijali. Mungu kila mara anawatafuta watu wanaomtaka. (Zaburi 14:2) Mungu atakuona tu. Tunaweza kusoma kwa upana kutoka kwa Daudi. Alikuwa shujaa mashuhuri, na alikuwa na uwezo wa kumwua Sauli na kuchukua ufalme kutoka kwake, lakini alimtii Mungu na akajaribu kila wakati kufanya kilichofaa. Yesu alisema yeyote anayejaribu kujiwekea uhai, kwamba ataupoteza, lakini atayemtumikia Mungu na maisha yake, atakuwa mwenye uhai. (Luka 9: 24) Daudi "alipoteza" maisha yake kwa kukosa kujitwika jukumu la ufalme. Lakini, baadaye baada ya miaka kadhaa, Mungu alimfanya kuwa mfalme wa Israeli, kama alivyomwahidi. Kwa njia kama hii, Yesu hakujitwika jukumu la ufalme, bali alimwacha Mungu kumtwika taji lile. (Wafilipi 2: 6-11) Siku moja Mfalme Sauli alipojaribu kumwua, Daudi alisema kitu fulani muhimu, usiimwage damu yangu mbali na uwepo wa Mungu. (1 Samueli 26:20) Kwa maneno mengine, hata ukiniua, kuwa na Mungu ndio jambo muhimu hata kuliko maisha yangu. Mungu alimrejelea Daudi kuwa mwanaume alitafuta Roho wa Mungu. (Samueli 13: 14, Matendo ya Mitume 13:22) Hili ni jambo nzuri sana Mungu kulisema kumhusu mtu! Hakuna mtu asiye na kasoro, na Mungu huwa anawaadhibu awapendao. (Waebrania 12:6) Siku moja, Daudi alimchukua mwanamke aliyekuwa ameolewa na kumtuma bwanake kwenye vita ili akafe. Jambo mbaya sana! Mungu alimtuma nabii Nathani ili amkashifu. Alimweleza hadithi kuhusu maskini

aliyekuwa na kondoo wa dhamana kubwa. Kisha jirani yake alimchukua kondoo yule na kumla hata ingawaje alikuwa na kondoo wengine wengi. Daudi alikasirika na kutaka Nathani auawe. Kama Peppy katika hadithi ya awali, tunapomwona mtu akikosea, tunakasirika, na hili linaonyesha kwamba pia wewe umekosa. (Roma 2:1) Muombe Mungu akusaidie kuichunguza roho yako na utubu. Kumbuka Sauli alipoambiwa makosa yake, hakuyakubali na akaendelea kukosea. Lakini Daudi alipoelezwa makosa yake, alikiri makosa yake, ni hii ni hatua ya kwanza katika kubadilika. Adhabu ya Mungu ilikuwa ni kuchukua uhai wa mwanawe Bethsheba. Daudi alimwomba Mungu aruhusu mtoto yule andelee kuishi. Tunaweza kumwomba Mungu kusitisha adhabu za dhambi zetu pia. Mara nyingine atakubali, lakini mara nyingine adhabu hii ni funzo kwetu na kwa wengine. Mtoto yule alifariki, lakini bado kulikuwa na matumaini. Mungu katika neema yake huwa anatumia tubu na kurejeshwa ili kuunda kitu kingine kizuri. Daudi na Bathsheba walipata mtoto mwingine aliyeitwa Solomoni. Mungu alimpenda Solomoni na ndiye alichukua ufalme na kuwa mzazi wa kale wa Yesu.

Naamua kuangazia roho yangu na kukubali adhabu ya Mungu.

### SULUHISHO LA 10



Karibia mwisho wa somo, Peppy alimwona msichana ambaye Peppy alichukua pesa zake akizitafuta mle darasani wakiandamana na mwalimu. Peppy alihisi vibaya sana, na alijua kwenye roho yake kwamba alifaa kukiri makosa yake, lakini alihisi vibaya hata zaidi kwa kumdhihaki mvulana yule, kwa kufanya jambo kama hilo. Mwishowe, hangeweza kuvumilia na alikiri kwa mwalimu na huyo msichana mwingine na kisha akazirudisha pesa zile. Kisha aliomba msamaha kwa mvulana yule kwa kumdhihaki siku mzima kuhusu kalamu zile za kuchora.

### SHUGHULI YA 10

**Roho**



Wanafunzi watatengeza umbo la Roho. Unaweza kutumia karatasi ngumu, na kupaka rangi au kutumia karatasi nyekundu. Pia, unaweza kutia karatasi ya plastiki juu ili kuifanya kudumu. Tia uzi kupitia shimo ili kuining'iniza. Umbo hili litakusaidia kukumbuka kwamba Mungu anaadhibu anaowapenda.

"Mungu ananiadhibu kwa sababu ananipenda."

### MSTARI WA 10 WA WAKATI


Je, Daudi alizaliwa mwaka gani? A. Hatujui kwa uhakika, lakini inakisiwa alizaliwa mwaka wa 1040 kabla ya Yesu.

Je, Daudi alifariki mwaka gani? A.Haijulikani halisi, lakini inakisiwa alifariki mwaka wa 970 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 10



| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| B | M | M | W | O | N | E | K | A | N | O |
| U | F | I | I | T | U | A | B | T | E | T |
| T | A | R | O | H | O | E | N | A | E | O |
| H | L | I | N | A | H | T | A | N | M | T |
| L | M | K | A | S | O | D | E | Z | A | M |
| B | E | T | H | L | E | H | E | M | U | R |
| I | L | T | T | D | H | A | M | B | G | O |
| B | A | T | U | F | A | M | A | K | A | P |
| B | M | F | B | M | W | B | P | C | H | H |
| P | D | A | U | D | I | I | I | U | C | O |



## MASWALI NA MAJIBU YA 10

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, Mungu pia huadhibu familia yote, miji, ama mataifa yote? Je, una mifano, (Ndio, Biblia inaeleza nyakati mbalimbali ambapo Mungu aliadhibu mji wote. Kwa mfano, Mungu aliadhibu Sodoma na Gomorra. Mfano mwingine ni wakati wanaisraeli walipotengeneza sanamu katika jangwa la Sinai, na Mungu alitaka kuwaadhibu wote. Musa aliomba huruma, na Mungu akisitisha adhabu. Musa aliichoma sanamu hii, akaweka vumbi ya dhahabu iliyoitengeneza kwenye maji na kuwapa watu wanywe kama adhabu! (Kitabu cha Kutoka 32). Wakati mmoja waliwaua takriban watu elfu 3, na wakati mwingine Mungu alisababisha pigo. Kuna mfano mwingine ambapo Mungu alimnyang'anya Mfalme Sauli na wanawe ufalme. Tunaweza kuzungumzia mataifa ya siku hizi ama miji au hata familia. Lakini makinika usije ukasema kila kitu kibaya ni adhabu. Yesu alisimulia kuhusu vitu vingi vilivyotendeka na kusema havikutendeka kwa sababu ya dhambi za watu. (Luka 13:1-5) Mungu ni mzuri sana kwetu na hivyo tunaweza kuomba rehema zake. Hata wakati tumetoka katika familia mbaya, ama mji au taifa mbaya… Mungu anatusaidia kutoka kwenye hali ngumu zisizofaa.)
2. Je, ni adhabu gani ya mwisho ulipokea, na kwa nini? (Zungumza kuhusu hali kila mtu alipitia.)
3. Kama polisi na wanasiasa wapo ili kuwaadhibu wanaokosea, basi mbona wale wabaya wamo huru na wanachukua pesa za wale wazuri? (Wazo hapa ni kuzungumza kwa pamoja kuhusu maovu yaliyo


ulimwenguni, na kwamba ni Mungu pekee anayeweza kutupa amani katika ulimwengu huu usio wa haki. Mtakachozungumzia kitategemea taifa ama eneo mlililoko.)

## MCHEZO WA 10



**Ukweli ama Uongo**

Mtoto mmoja atasimama na kusema fungu fulani la maneno kama vile "Jonah alitengeneza Safina" na wanafunzi watajibu kama ni Kweli au Uongo. Kama watafikiri ni ukweli basi watainua kidole chao cha gumba, kama watafikiri ni uongo basi watakielekeza chini. Watakaokosea watakimbia zamu moja kuzunguka kikundi au eneo la kuketi na kisha kutafuta mahali pa kuketi wakirudi. Mwenye atakosa mahali pa kuketi, ndiye atakayesema fungu linguine la maneno.




## MAHUDHURIO YA 10

Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Daudi**

## KAZI YA 10 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kariri kifungu hiki,"Mungu huniadhibu kwa sababu ananipenda." Wakati mzazi au mwalimu wako anakuadhibu kwa kosa ulilofanya, kumbuka kifungu hiki: "Mungu huniadhibu kwa sababu ananipenda." Lakini ukijipata unawaza,"Lakini siwezi kufanya kosa! Sikulifanya kimakusudi!" Chunguza ulichokifanya tena, na uzingatie matendo yako halisi, lakini sio kusudi. Kubali matokeo bila kujitetea.

**Soma**

Siku ya 1: 1 Wafalme 5:1-5
Siku ya 2: 1 Wafalme 6:1-2, 14
Siku ya 3: 1 Wafalme 7:48-51
Siku ya 4: 1 Wafalme 8:22-26
Siku ya 5: 1 Wafalme 8:27-30

# 11.HEKALU YA MUNGU



**Haditi ya Biblia: Mfalme Solomoni**
1 Kitabu cha Wafalme 2:1-4, 3:4-15, 4:29-34, 6:1, 6:37-38, 8:1-8:30

## FUNGU LA 11 LA KUMBUKUMBU

"Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?" 1 Wakorintho 3:16



## HADITHI YA 11 YA UHITAJI

Buzz alimwona rafiki yake mmoja akivuta sigara na rafikiye alimwalika kuvuta naye…

## SOMO KUU LA 11

Mfalme Daudi katika hadithi ya wiki iliyopita alitaka kumtukuza Mungu kwa kujenga hekalu nzuri na maarufu, lakini kwa sababu alikuwa ni mpiganaji katika vita, hakuruhusiwa na Mungu. Badala yake, Mungu alimwahidi kwamba mwanawe angeijenga na akadhibitisha ahadi hio mara mbili. Mwanawe Daudi, Solomoni, akawa mfalme wa Israeli. Siku moja alitoa dhabihu elfu moja, kwa Mungu. Yohana 4:8 inasema kwamba tunapomkaribia Mungu, naye pia anatukaribia. Usiku huo, Mungu alimtaka Solomoni kusema chochote alichokitaka. Je, unaweza kuomba gari nyekundu la kifahari? Nguo nzuri? Lakini badala yake, Solomoni aliomba maarifa ya kuwaongoza watu wake. Lo! Mungu aliridhishwa na jambo hili! Alimfanya Solomoni kuwa mtu mwenye maarifa zaidi kuliko yeyote ambaye amewahi kuishi na akambariki na utajiri na ushindi. Solomoni alijenga hekalu nzuri sana ya mawe na ndani ilijaa michongo. Fikiria chumba cha dhahabu, na ndani kulikuwemo vifaa vya kuwekelea mishumaa vyenye ukubwa zaidi mithili ya mtu. Solomoni alitangaza sherehe za siku 14 ili kuisherehekea hekalu hii. Utukufu na uwepo wa Mungu uliingia ndani kama wingu leusi. Walitoa ng'ombe 22,000 na kondoo na mbuzi 120,000 kama dhabihu. Halafu Solomoni aliomba, ila hakujiombea, bali aliwaombea watu wa Mungu.

Hekalu hio haipo tena, na ya pili pia, lakini Mungu alitimiza ahadi yake kutumia hekalu nyingine nzuri hata zaidi. Akiwa hapa ulimwenguni, Yesu alisema angeibomoa hekalu na kisha kuijenga kwa siku tatu. (Yohana 2: 19) Hakuwa anaizungumzia hekalu ya kujengwa kimwili bali hekalu ya kiroho ambayo alijenga kupitia kufariki na kufufuka kwake. Je, unaweza kuiona hekalu hio mpya hii leo? Kweli, lakini sio jumba la kanisa. WEWE (Kwa wingi) ni hekalu ya Mungu! (Waefeso 2:19- 22) Sisi Wakiristo ni kama mawe ya kujenga. Roho wa Mungu anaishi ndani yetu, kama vile wingu leusi lililoingia kwenye hekalu, na sisi sote kwa ujumla tunaunda hekalu ya kiroho ambamo Mungu anaishi wakati wote.

Mungu anaendelea kuijenga na kuifanya kuwa hata nzuri zaidi na ametualika kumsaidia. Unapowaambia wanafunzi wenzako kumhusu au hata kuzungumza kuhusu Yesu kanisani, unasaidia kuijenga. Inagharimu maarifa kusaidia Mungu kuijenga vinavyofaa. Maarifa ya mfalme Solomoni yalijulikana sana hadi na Malkia Sheba, alimtembelea ili amsikie akizungumza, lakini Yesu anamshinda Solomoni. (Mathayo 12:42) Yesu ndiye chanzo cha maarifa yetu na atatupa maarifa tunapomwomba. (Yakobo 1:5). Unapofanya mtu mwingine kufanya dhambi, mnajenga kitu kisicho imara na kisichopendeza. (1 Wakorintho 3: 10-15)

Tunapohimizana kuwa wenye wema hata kwa watu wasio wema, unasaidia kuifanya iwe hata nzuri zaidi. Yesu alitwambia tupendane, kama alivyotupenda. (Yohana 13:34) Kama dhahabu, uzuri upo katika vile tunavyowatenda wengine. Yesu alisema Hekalu inaifanya dhahabu kuwa na uungu. (Mathayo 23 17) Wasiomwamini Yesu wanaweza kuwa na wema kama dhahabu, lakini kumwamini Yesu pekee ndio kunakufanya kuwa kiungo cha hekalu.

Nitamwomba Mungu kunipa maarifa, ili nisaidie kuijenga hekalu yake kwa kuwapenda wengine.

## SULUHISHO LA 11

Buzz alijua kwamba haya yalikuwa ni makosa akasema, “Rafiki, usifanye hivyo, lazima uchunge mwili wako, kwa sababu kuvuta sigara kunadhuru viungo vya mwili na kunafupisha maisha yako. Zaidi, mwili wako ni hekalu ya Roho Mtakatifu, Mungu anaishi ndani yako, na lazima uchunge mwili wako na kumtii Mungu.”



## SHUGHULI YA 11

**Ulengaji na Mashimelo**

Kwa hii, utahitaji chupa za plastiki au vikombe, puto na au mipira ya karatasi. Kitu cha kwanza kufanya ni kukata upande wa chini wa vikombe. Kisha ukate kipande kidogo cha upande wa juu wa puto. Kisha ufunge funda upande wa chini wa puto, na kisha uivute na kufunika hadi mwisho wa kikombe na kuifunga. Mwisho wa kikombe utaiweka puto mahali inafaa. Halafu weka mipira ya karatasi ndani ya kikombe, halafu uvute na kuiwachilia ili kutupa karatasi. Shindaneni na kuona nani atakayetupa mbali.



## MSTARI WA 11 WA WAKATI

Je, Solomoni alizaliwa mwaka gani? A.Hatujui kwa uhakika lakini inakisiwa alizaliwa mwaka wa 989 kabla ya Yesu. Je, Solomoni alifariki mwaka gani? A. Hatujui kwa hakika, lakini inakisiwa alifariki mwaka wa 931 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 11





| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U | H | O | S | O | L | O | M | O | N | I |
| L | O | R | U | I | D | A | T | H | A | B |
| A | E | O | J | H | B | S | O | E | L | I |
| K | M | H | E | K | I | M | A | K | I | B |
| E | L | O | M | R | I | B | O | A | D | L |
| H | A | O | I | R | I | J | A | T | U | I |
| M | F | K | M | O | I | D | A | H | A | A |
| J | M | F | U | B | A | H | A | H | D | T |
| I | J | E | N | G | A | M | K | R | I | S |


## MASWALI NA MAJIBU YA 11

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, ni kwa njia gani tunazoweza kulinda miili na mioyo yetu? (Taja vitu vya kimwili, kama vile kutovuta sigara, kutotumia dawa za kulevya, kungoja hadi tuolewe ili kushiriki ngono, na kumakinika ili tusitizame picha zisizofaa. Pia taja baadhi ya vitu vinavyohusisha roho kama vile kuwasamehe wengine, kuwapa wengine heshima na upendo, kutubu dhambi, na kuwa na mtazamo mzuri. Njia nzuri ya kushinda dhambi kubwa ni kuzikiri kwa mhubiri au mwalimu, na kuwaomba wakusaidie katika maombi na pia wakusaidie. Kwa mfano, uanweza kuwaomba wakuulize kila wiki jinsi unavyokabiliana kibinafsi na dhambi fulani.)
2. Je, kuwa Mkristo inaleta furaha? (Bila shaka! Ila ni furaha tofauti. Sio furaha ya kucheza densi na mvulana mpya na kuhisi vipepeo mwilini. Ni tofauti, ni furaha, amani na uhuru ambao hauwezi patikana katika ulimwengu.)
3. Mbona wazazi wangu huniambia HAPANA kila wakati? (Kwa sababu wanataka kukulinda.)


## MCHEZO WA 11

**Simu Iliyovunjika**



Unda timu mbili ambazo watasimama katika safu mbili. Kisha mwalimu atamwambia mtu wa kwanza katika kila safu fungu Fulani la maneno, nan aye mtu huyu atamwambia mwenzake katika safu fungu hili. Timu ambayo mwishoni itakuwa na fungu linalofanana na fungu la mwanzo, itashinda.

## MAHUDHURIO YA 11




Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Salomoni**

## KAZI YA 11 YA NYUMBANI

**Kazi**

Kazi yako ya ziada ni kumpa moyo mtu Fulani kila siku katika wiki hii, hasa mtu anayeenda kanisa tofauti na unaloenda. Ukiona mtu akitenda wema, mpe pongezi. Ukiona motto mwingine anayemwamini Yesu akitenda lisilofaa, mkumbushe kwa njia ifaayo afanye linalofaa: Usimwambie “Wewe ni mbaya” ila mwambie” unapotenda hilo humridhishi Mungu. Labda unaweza kufanya hili badala yake.” Na utoe mfano wa jambo nzuri analoweza kufanya. Ziada: Soma ujumbe katika mlima katika kitabu cha Mathayo 5-7.

**Soma**

Siku ya 1: 1 Wafalme 17:1-6
Siku ya 2: 1 Wafalme 17:7-11
Siku ya 3: 1 Wafalme 17:12-16
Siku ya 4: 1 Wafalme 17:17-19
Siku ya 5: 1 Wafalme 17:20-24

# 12. MUNGU HUTUONA



**Hadithi ya Biblia: Eliya**
1 Wafalme 17:1-24

## FUNGU LA 12 LA KUMBUKUMBU

" Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa." Matayo 6:33

## HADITHI YA 12 YA UHITAJI



Siku moja Taffy aliamka mwenye furaha. Siku ile alitaka kufanya kitu maalum ili kumdhihirishia mama yake jinsi alivyompenda. Alikwenda kwenye shamba, akavuna maua yaliyokuwa mazuri zaidi na kisha akayaweka mahali mama yake angependa, kisha akaenda jikoni kutayarisha kiamsha kinywa. "Hiki kitakuwa ndicho kitamu zaidi," Alisema Taffy, huku akipanga kila kitu kwa njia maalum.

Mwishowe, mama yake aliamka. Taffy alimngoja mezani huku kila kitu kikiwa tayari. Mama yake alipotoka… Hata hakuyatizama maua yale au kumsalimu Taffy. Aliketi chini na kula kiamsha kinywa na hakumshukuru Taffy alipomaliza.

Taffy alikasirika, na akajifungia kwenye chumba chake, na akadhani mamake hampendi.

## SOMO KUU LA 12

Karibu tena katika Mashujaa wa Imani! Wakati uliopita, tulisoma kuhusu hekalu ya Solomoni. Baadaye, ufalme uligawanywa mara mbili, Israeli na Yuda. Baadaye, Mfalme Ahabu pamoja na mkewe Jezebeli walitawala Israeli. Kwa sababu ya dhambi zao, Mungu alimtuma nabii aliyeitwa Eliya na habari kwamba hakungenyesha kwa miaka kadhaa. Wakati huo wote, Eliya alijificha katika korongo. Mungu anaona tunachopitia, hata kama hakuna mwingine anayeona, kama Taffy katika hadithi ya awali. Hakuna jambo utatendea wengine ambalo halitatambulika. Na Mungu atatupa tunachokihitaji, na ili kufanya hivyo, hahitaji fedha wala njia za kawaida. Mungu alimpa Eliya maji kutoka kwa kijito, na akawatuma kunguru na mkate na nyama mara mbili kwa siku. Fikiria ndege akiburuka hadi ulipo na kisha kukupa mkate! Yesu alitwambia tusiwe wenye wasiwasi kwani Mungu anawalisha hadi ndege. (Mathayo 6:26)

Na katika hadithi hii, Mungu aliwatumia ndege ili kumlisha Eliya. Kijito kilipokauka, Mungu alimtuma Eliya katika sehemu ambayo hakuitarajia, si kwa tajiri mbali kwa mjane mgeni. Eliya alipomwomba mkate, alisema kwamba alikuwa na unga wa ngano kiasi kidogo mno na pia mafuta ya kupikia kiwango kidogo mno, na kwamba alifikiria familia yake ingefariki baada ya vitu hivi kuisha. Je, ushawahi kuucheza mchezo wa kuaminiana ambapo unajiangusha upande wa nyuma, na kisha rafiki yako anakushikilia kabla ya wewe kuanguka? (Jaribu na atakayejitolea) Mara nyingine Mungu anangoja hadi wakati wa mwisho, ile siku kabla umeishiwa, kwa sababu anajua itaongeza imani na tumaini kwake. Eliya alimwambia mjane asiingiwe na wasiwasi ila tu amtengenezee mkate. Kwa njia kama hii, Yesu anatwambia kwanza tuutafute ufalme wa Mungu na kwamba atatupa kila tunachokihitaji. (Mathayo 6:33) Unga na mafuta yake kwa muujiza hayakuisha, walikuwa na mkate wa kula wakati wote. Je, unapokuwa na maswali kama, "Nitatoa wapi vyakula wiki hii?" "Nitapata wapi nguo ninazohitaji shuleni?" Tizama na uone jinsi

Mungu atakavyokupa. Kisha umweleze mtu kuhusu jambo hili na kisha uliandike ili ilikumbuke baadaye. Je, ushawahi kushuhudia Mungu akikupa? (Toa nafasi kwa hadithi fupi za ushuhuda.)

Mungu hapeani vyakula na nguo pekee, bali pia uhai. Mwana wa mjane yule akakuwa mgonjwa na akafariki, na Eliya alimchukua mvulana yule na kuomba mara tatu. Unaweza kuombea familia na marafiki zako hata wasipokuamini, na sio mara moja bali waombee mara kadhaa. Baada ya Eliya kuomba mara ya tatu, Mungu alimfufua mvulana yule! Yesu alifariki na kufufuka na sasa yupo hai milele na milele. Hata kama miili yetu inafariki, kila mtu ana roho inayoishi milele. Yesu alisema adui yuaja kuiba, kuua, na kuharibu, lakini Yesu alikuja ili tuwe na maisha yaliyojaa neema. (Yohana 10: 10) Kupitia Yesu Kristo, unaweza kuishi milele mbinguni na Mungu.

Naamini kwamba Mungu ananiona. Mungu ananipenda na atanipa chochote ninachohitaji.

## SULUHISHO LA 12



Siku ifuatayo katika shule ya watoto kanisani, walisoma kwamba Mungu anaona kila mahali. Mwalimu darasani alimpa kila mwanafunzi ua. Taffy aligundua kwamba Mungu alikuwa akizungumza naye na kumwambia "Hongera" kwa sababu ya alichomfanyia mama yake.

## SHUGHULI YA 12

**Habari ya Asubuhi Mungu**




Katika kijikaratasi, wewe na watoto mtaandika fungu la maneno "Habari ya asubuhi Mungu" Pamba na kalamu za kuchora. Watoto watakibandika katika dari au kuta zilizoko mbele ya vitanda vyao. Jukumu ni kusoma kila asubuhi na kumwambia Mungu, "Habari ya asubuhi Mungu." Hii itawakumbusha kwamba Mungu yupo nao kila wakati.

## MSTARI WA 12 WA WAKATI

Je, matukio ya Eliya na mjane yalifanyika lini? A. Karibia mwaka wa 868 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 12





| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | A | F | U | T | A | F | U | H | V | Y | A | K | U |
| A | N | A | K | I | L | U | J | U | K | A | L | I | B |
| H | M | K | A | T | N | F | U | P | U | O | U | L | A |
| I | U | R | U | G | N | U | K | E | N | T | K | A | M |
| T | E | F | A | B | I | L | A | A | G | O | A | A | A |
| A | N | O | T | I | J | I | K | N | R | J | Y | H | H |
| J | A | U | F | V | Y | W | S | A | A | I | V | S | I |
| I | J | O | H | I | F | A | R | H | L | K | U | O | T |
| U | M | E | T | A | K | M | U | E | M | T | O | T | O |

## MASWALI NA MAJIBU YA 12

**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, kuna wakati ambapo Mungu aliwahi kukupa ulichokiomba? Shiriki ushuhuda wako. (Toa muda wa kutosha ili wanafunzi washiriki.)
2. Je, mbona Mungu aliniumba? (Zungumza kuhusu upendo wa Mungu, kuhusu njia tofauti za kumtumikia, na jinsi Mungu anavyokujua kukuhusu ikiwa ni pamoja na ujuzi, vipaji, unachopenda na hisia zako.)
3. Kama Mungu anaona kila kitu, anaona hadi makosa yetu. Je, unahisi vipi unapopatikana ukifanya jambo lisilofaa? Katika hali kama hio, je, umekiri makosa yako? (Zungumza kuhusu hali na jinsi ilivyo vigumu kukiri makosa. Usiwaruhusu waseme kwamba hawafanyi makosa na kwamba hawajawahi patikana kwenye kosa, kwa sababu huo ni uongo!)






## MCHEZO WA 12

**Toboa Puto!**



1. Kwanza, fungilia puto iliyojaa hewa katika kifundo cha mguu cha kila mtoto.
2. Cheza mziki na kuwaalika wacheze katikati mwa darasa.
3. Kila mwanafunzi anafaa kujaribu kuitoboa puto ya mwenzake huku akimakinika yake isitoboke.
4. Kila mwanafunzi ambaye puto yake itatoboka atatoka kwenye mchezo.

**Lengo:** Toboa puto ya wengine bila kuwakubalisha kuitoboa yako.




## MAHUDHURIO YA 12

Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Eliya**

## KAZI YA 12 YA NYUMBANI

**Kazi**

Andika kifungu hiki, "Habari ya asubuhi, Mungu Mkuu" katika kipande cha karatasi na ukiweke karibu na mahali utakiona kila unapoamka asubuhi. Hili litakukumbusha kwamba Mungu anakuona wakati wote. Kama utakosa chochote wiki hii, omba Mungu akupe. Tizama jinsi Mungu anavyopeana na umwambie mwalimu wako kuhusu hili wakati ufuatao.

**Soma**

Siku ya 1: 1 Wafalme 18:16-21
Siku ya 2: 1 Wafalme 18:22-26
Siku ya 3: 1 Wafalme 18:27-35
Siku ya 4: 1 Wafalme 18:36-39
Siku ya 5: 1 Wafalme 18:40-46

# 13.MUNGU WA PEKEE



**Haditi ya Biblia: Eliya na Manabii**
1 Wafalme 18:16-46

## FUNGU LA 13 LA KUMBUKUMBU

"Ee BWANA, wewe u Mungu wangu; Nitakutukuza na kulihimidi jina lako; Kwa kuwa umetenda mambo ya ajabu, Mashauri ya kale, kwa uaminifu na kweli." Isaya 25:1

## HADITHI YA 13 YA UHITAJI



Siku moja shuleni, Kip aligundua kwamba mwalimu wake wa shuleni, alikuwa ni mgonjwa. Kip alimwambia kwamba alijua mtu ambaye angemponya. Mwalimu alisema, "Usijali, nilikwenda kwa mwanamke fulani na alifanya tambiko na kunipa dawa ya kuniponya. Tayari najihisi nafuu." Mwalimu alikataa usaidizi wa Kip….

## SOMO KUU LA 13

Wakati uliopita tulisoma kuhusu nabii Eliya. Wakati huo, Israeli ilkuwa ikijaribu kuabudu miungu tofauti wakati mmoja. Lakini Mungu hataki tuabudu miungu mingine, kwa sababu yeye ndiye Mungu pekee. Yesu alisema kwamba hatuwezi kuwafuata bwana wawili, kwani tutamchukia mmoja na kumpenda mwingine au kumfuata mwingine na kumuasi mwingine. (Mathayo 6:24) Nabii Eliya aliwaleta wanaisraeli na manabii wote wa miungu ya sanamu katika mlima wa Karmeli. Aliiambia Israeli kuchagua Mungu halisi wa kumwabudu. Aliwaambia manabii wa Baali watengeneze dhabahu na kutayarisha sadaka, na Eliya angefanya vile vile kwa Mungu wetu. Mungu ambaye angejibu kwa moto angekuwa ndiye Mungu wa ukweli. Tulishuhudia jambo kama hili na mwalimu wa Kip.

Manabii wa Baali walifanya kama alivyotaka Eliya, lakini hawakujibiwa. Baada ya muda, Eliya aliwauliza kwani Mungu wao alikuwa amelala, ama alikuwa safarini au katika shughuli. Hatufai kuingiwa na wasiwasi kwani Mungu wetu wa ukweli halali, wala hasafiri kwani yupo mahali pote kila wakati, na ni mwenye maarifa sana na anaweza kuongoza ulimwengu wote mara moja. Baali, mungu huyo mwingine hakujibu wala kutuma moto wowote. Kisha adhuhuri, Eliya alitayarisha sadaka yake. Alijenga madhabahu na kuweka sadaka yake juu, kisha aliimwagia maji ili kuifanya ngumu kuichoma kwa moto. Akawaagiza wamwagie maji hadi ikaloa na kujaza maji mtaro uliokuwepo karibu na madhabahu. Haijalisha jambo ni ngumu kwa kiasi gani, Mungu wetu ni mwenye nguvu zote, na anaweza kufanya lolote. Eliya aliomba, na Mungu alimjibu mara moja na kuutuma moto kutoka mbinguni!

Moto huo ulichoma sadaka yote pamoja na mawe na maji na pia vumbi ilikuwepo karibu. Yesu alisema kwamba yeye ndiye njia kufika kwa Mungu, kwamba yeye ndiye ukweli na uhai. (Yohana 14:6) Hakuna njia nyingine mbinguni bali kupitia Yesu, kwa sababu hakuna miungu mingine bali Mungu mmoja tu. Kumwabudu Mungu tu inamaanisha kutofuata dini nyingine wala miungu mingine. Lakini kuna kitu kingine ambacho kinaweza kututia katika mtego. Baada ya Yesu kusema kuwa hatuwezi kuwa na mabwana wawili, alizungumza kuhusu kitu kingine ambacho watu wanakiabudu. Yesu alisema hatuwezi kuabudu Mungu na pesa. (Mathayo 6: 24) Ni rahisi kutaka nguo zingine nzuri, gari nzuri, nyumba, kichezea, na hadhi. Unaweza kuwa na vitu hivi mara nyingine, lakini usiruhusu vitu vingine kuwa vyenye

umuhimu kuliko Mungu. Badala yake, vitumie kumwabudu Mungu na kuwatumikia watu wake. Kumbuka wakati uliopita, tulisoma jinsi ya kutafuta kwanza ufalme wake na kumwamini Mungu kwamba atatulinda. (Mathayo 6: 33) Yesu alisema tunafaa kumwabudu Mungu na yeye pekee. (Luka 4:8)

Nachagua kumwabudu Mungu wa ukweli na kumweka mbele katika maisha yangu.

## SULUHISHO LA 13


Muda mfupi ulipita, na mwalimu aliendelea kupata nafuu, lakini hakuwa na afya. Siku ilifika ambapo alikuwa mgonjwa zaidi na akakumbuka Kip na kumwongelesha. Kip, alimpeleka mhubiri wake kwa mwalimu wake. Walimwombea, na alipona kabisa. Mwalimu alimkubali Yesu maishani mwake na kutambua kwamba nguvu zote ni za Mungu.



## SHUGHULI YA 13

**Lebo ya Utambulisho**

Kata umbo kwa kila motto kulingana na ilivyoonyeshwa. Kila mtu ataweka maelezo yake kama ilivyoonyeshwa kwenye picha na kisha kutia karatasi ya plastiki juu ili kulifanya lidumu. Tia kijinyororo, riboni au kamba na kuivaa shingoni. Itakusaidia kukumbuka kwamba, Yesu ndiye anayekumiliki na wewe ni wake.






“**Namilikiwa na Mungu**

Jina: Robert

Rangi ninayopenda: Bluu


Chakula ninachopenda: mkate mtamu”

## MSTARI WA 13 WA WAKATI

Je, ni mwaka gani matukio ya Eliya na manabii yalifanyika? A. Takriban mwaka wa 866 kabla ya Yesu.

## MAJIBU YA MAFUMBO YA 13






| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | I | L | E | M | R | A | K | G | O | J | I |
| L | A | I | U | H | I | B | A | H | D | O | I |
| I | I | J | L | A | M | U | N | G | N | T | B |
| M | K | Y | I | A | B | D | U | D | E | O | A |
| A | I | N | I | M | A | U | L | A | P | M | N |
| Y | M | A | D | H | A | B | A | H | U | W | A |
| E | U | V | U | G | N | E | Y | N | E | W | M |
| M | T | A | R | O | M | A | G | B | A | L | I |
| K | A | R | M | E | L | U | A | Y | I | L | E |

## MASWALI NA MAJIBU YA 13


**(Kwa wanafunzi wakubwa)**

1. Je, ni vitu gani tunajaribiwa kutumikia au kuabudu mbali na Mungu mwenyewe? (Katika sehemu kadhaa, kuna jaribio la kuabudu miungu mingine, kwa mfano, ambapo watu hawapendi kuwa Wakiristo au pale familia inapokusukuma sana au wakati wa tamasha shuleni. Pia kuna majaribu ya kutumikia vitu vingine, kwa mfano, pesa, umaarufu, kupendwa, urembo, vyakula, cheo, maringo, uchoyo, nk. Jadiliana mifano.)
2. Je, miungu mingine katika dini zingine huwa nini? (Biblia inasema kuwa hio si miungu haswa, bali ni mapepo yanayojaribu kuwadanganya watu na kuwavuta mbali na Mungu Yule mmoja. Biblia pia inasema kwamba mungu atahukumu miungu hio mingine, yaani mapepo, na yatarushwa katika ziwa la moto. Sisi tulioweka imani yetu na kumwamini Mungu, tutaishi Naye mbinguni milele. Mungu anatuambia mara nyingi katika Biblia kwamba hatufai kuogopa: na kwamba Yule tunayefaa kumwogopa katika ulimwengu wote ni Yeye pekee, na kwamba yupo katika upande wetu na anatupenda. (1 Wakorintho 10:20, Mathayo 10: 28-31, Zaburi 103:13, Warumi 8:13)

3. Je, naweza kuwacha kumwabudu Mungu kwa muda? (Kuamini Mungu na kumtumikia sio jambo la kufanya siku moja halafu kutolifanya siku nyingine. Zungumza kuhusu watu (bila kutaja majina yao) ambao umeona wakiwaacha kumwabudu Mungu kwa muda.)

## MCHEZO WA 13

**Mbio za Kupokezana**



Unda timu mbili, na wasimame katika mistari miwili katika upande mmoja wa eneo mnakochezea. Mmoja kwa mwingine, wachezaji wataruka kwa mguu mmoja na kuweka neno moja (au herufi iwapo kuna watoto wa kutosha) la fungu la maneno, "Tutamwabudu Mungu pekee." Timu itakayomaliza kifungu hiki ikiwa ya kwanza, itaibuka mshindi.

## MAHUDHURIO YA 13




Wape wanafunzi kadi ya leo kwa kuhudhuria darasa. Wapongeze na uwahimize wahudhurie wiki ijayo ili wapate kadi nyingine ya kuwawezesha kucheza mchezo wa Mashujaa! Kadi ya leo ni:
**Moto wa Mungu**

## KAZI YA 13 YA NYUMBANI

**Kazi**

Waza kuhusu kitu unachokipenda sana, kama vile kipenzi, nguo, mfuko, pesa, na kadhalika. Waza kuhusu jinsi unaweza ukamtumkia Mungu au kumfaidi mtu mwingine na kitu hiki. Kama ni kipenzi, unaweza kumpa mtu mwingine na kumruhusu kucheza nacho. Kama ni mavazi na una dada au kaka mdogo anayeweza kuyavaa, mpe avae. Kama ni pesa zitoe kwa kanisa au kwa mtu anayezihitaji. Kama sio kitu kinchoweza kuguswa, kwa mfano talanta ama mpango wa kudurusu, omba Mungu na umwambie, "Mungu, hii talanta, masomo, ujuzi, ndoto, na kadhalika ni yangu. Tafadhali nisaidie kujua ni jinsi ninavyoweza kuitumia ili kukutumikia au kuwafaidi wengine. Ziada: kama unaishi katika hali ambayo famlia au jamii yako inaabudu mungu tofauti, jaribu usijihusishe. Kama unalazimishwa kushiriki, muombe Mungu na umpe roho yako yote na umwombe akulinde na akusaidie katika hali hii. Mungu, ambaye ni mkubwa na mwenye nguvu kuliko chochote au mtu yeyote, anaiona roho yako.

**Soma**

Kazi ya ziada isiyo ya kusoma

Héroes 2 Teacher
Swahili
12032

www.ChildrenAreImportant.com
info@childrenareimportant.com
We are located in Mexico.
00-52-592-924-9041

Watoto ni wa muhimu